**BASTOLA** iliyoibwa nyumbani kwa Nape yakamatwa Mbeya

UKURASA 4



**FAMILIA** yatoa masharti maziko ya Jaji Mwaikasu

UKURASA 4


Jicho na mfumo ukusanyaji pesa za serikali usipoteza hata 'senti'
Ljue zao mpunga, namna ilivyo kinara wa uchumi
BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe
Waziri Mkuu awakumbatia Machinga na darasa la jicho, miwani ya Serikali kwao
• Wanabeba robo nguvu kazi, pato taifa

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Februari 19, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580496

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# Ujumbe wa mwisho aliotoa Maalim Seif



**AZIKWA** rasmi Pemba, vilio, simanzi vyatawala kila kona... *Endelea Uk. 2*



Umati wa wananchi wa Zanzibar, ukiwa katika viwanja vya Mnazi Mmoja, wakisubiri kuusalia mwili wa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad. Picha ndogo, maofisa waandamizi wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili huo, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume. **PICHA ZAIDI UK. 19. PICHA: IKULU**






## Magufuli kuongoza kuagwa kwa Balozi Kijazi

UKURASA 3



## TEC yatoa utaratibu mpya wa ibada na mikusanyiko

UKURASA 3

**MICHEZO** MTIBWA YALIA UWANJA WA JAMHURI KAMA WA UGENINI UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# ...Vilio, simanzi vyatawala

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, jana aliongoza maziko ya Makamu wa Pili wa Rais wa visiwa hivyo, Maalim Seif Sharif Hamad, huku vilio na simanzi vikitawala wakati mwili wake ukiwasili kisiwani Pemba.

Wakati hayo yakitokea, baadhi ya wananchi walisema wamepokea kwa mshtuko taarifa ya kifo chake na kwamba hawatamsahau kwa mchango wake wa kuwaweka pamoja katika kudumisha amani na mshikamano.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, walisema Maalim Seif alikuwa anapenda kutetea maslahi ya wananchi wa Zanzibar kipindi cha uhai wake na kwamba hakuchoka kupigania mpaka umauti kumfika.

Kutokana na hali hiyo, walisema watamkumbuka Maalim Seif kwa mchango wake mkubwa wa kutetea haki zao na kamwe hawatoacha kumwombe dua.

Walisema Maalim Seif alikuwa mtu jasiri, mpiganaji na asiyechoka na mwenye huruma. Licha ya vikwazo alivyokuwa akikumbana navyo, hakukata tamaa, tutamuenzi na kumwombea dua kila siku.

Mkazi wa Chakechake, Asha Abdalla Hamad, alisema wameumia sana kuondoka kwa Maalim Seif, ingawa kitu kinachowapa faraja ni kule kuwaweka pamoja wananchi wa Zanzibar.

Maalim Seif alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam, alikokuwa akipatiwa matibabu na alizikwa kijijini kwao Mtambwe, Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**MWINYI AONGOZA MAZIKO**

Rais Dk. Mwinyi, jana aliongoza mamia ya wananchi wakiwamo viongozi kwenye ye maziko ya Maalim Seif, Mtambwe kisiwani Pemba.

Kabla ya maziko, jana asubuhi mwili wa Maalim Seif ulichukuliwa Muhimbili na kupelekwa msikiti wa Maamur, Upanga, jijini Dar es Salaam kwa ajili ya dua.

Baada ya dua, mwili huo ulipelekwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ukiwa kwenye gari maalum la Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na ulipofika, maofisa waandamizi wa JWTZ waliubeba na kuuingiza kwenye helikopta ya Jeshi namba JW-9509.

**PEMBA**

Baada ya kuwasili visiwani Pemba ulipelekwa moja kwa moja katika uwanja wa Gombani kwa kutumia gari maalum la jeshi na wanajeshi waliutoa na kuupeleka moja kwa moja katika eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya sala na baadaye kijijini kwao Mtambwe.

Wakati gari lililobeba mwili wa Maalim Seif likipita kijijini humo, vilio na simanzi vilitawala wakati wote huku wanawake wakiwa wamekaa chini wengine walionekana wakisoma dua.

Mwili huo ulipelekwa msikitini kijijini Mtambwe na baada ya sala uliondolewa na kupelekwa eneo lililotengwa kwa ajili ya maziko.




Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, akiaga mwili wa aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Mhandisi John Kijazi, katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ujumbe wa mwisho wa Maalim Seif huu

**Na Romana Mallya**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amebainisha mambo aliyoongea na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad siku moja kabla ya kulazwa hospitalini.

Maalim Seif ambaye alikuwa Mwenyekiti wa chama hicho, alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), alikokuwa akiendelea na matibabu.

Katika hotuba yake aliyoisoma baada ya mazishi ya kiongozi huyo yaliyofanyika jana alasiri Mtambwe visiwani Pemba, Zitto alisema kuwa siku moja kabla Maalim Seif kuanza kuumwa, alifanya mazungumzo naye ofisi kwake.

"Pamoja na mambo mengine, alinisisitiza sasa kuhakikisha kuwa vyovyote iwavyo, chama chetu kinakuwa mstari wa mbele kuimarisha maridhiano. "Sikujua kumbe alikuwa ananiaga. Ninafahamu kuwa siku hiyo, alikutana pia na mawaziri wawili wa Serikali ya Zanzibar, sijui wenzangu hao wosia wao ulikuwa nini," alisema.

Zitto alisema mwisho wa Maalim Seif duniani, siyo mwisho wa mawazo na fikra zake, bali ni mwanzo wa kutekeleza maono yake kwa aina ya Zanzibar aliyopenda kuijenga pamoja na Wazanzibar wote.

Alisema wana matumaini makubwa kwamba maono yake ya kuifanya Zanzibar kuwa Singapore ya Afrika, yatatimia muda siyo mrefu kutoka sasa. "Umoja wa Kitaifa utaendelea kuenziwa na haki kwa kila Mzanzibar kutolewa bila ubaguzi. ACT-Wazalendo tutaendelea kutoa mchango kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili kuhakikisha ndoto ya Maalim Seif ya kuleta ustawi wa Zanzibar, haki kwa Wazanzibar na umoja wa Wazanzibar haizimiki," alisema. Zitto alisema msiba huo siyo tu mzito kwa Zanzibar, bali pia kwa chama chao na wapigania demokrasia ndani na nje ya nchi.

"Maalim Seif alikuwa ni baba wa demokrasia ya vyama vingi nchini, mlezi wa vijana wanaochipukia katika siasa za vyama vingi, muumini mkubwa wa ustawi wa wananchi wa Zanzibar na mpambania haki za wananchi wote bila kujali itikadi na imani zao," alisema.

Kiongozi huyo alisema wamempoteza mtu muhimu katika malezi ya kisiasa na mshauri mahiri, mpatanishi kwenye vikao vya chama na aliyewapa ujasiri wa kusonga mbele pale walipokaribia kukata tamaa kutokana na mazingira magumu ya kisiasa katika siku za karibuni.

"Tulipokaribia kukata tamaa au kukatishwa tamaa, tulijikumbusha mapito magumu aliyopitia Maalim Seif katika mapambano ya kudai haki, heshima na ustawi wa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

"Kila tulipojikumbusha mapito ya Maalim Seif, tunajiona bado tunayo nguvu kubwa ya kusonga mbele zaidi katika mapambano ya kudai haki na ustawi wa wananchi," alisema.

Zitto alisema pamoja na ajali mbalimbali za kisiasa alizokutana nazo wakati wa uhai wake, Maalim Seif hakuwahi kukata tamaa, kuyumba wala kuyumbishwa katika jambo alililoliamini.

"Aliyaishi maneno yake aliyoyasema mwezi Desemba mwaka 1987 katika viwanja vya Tibirinzi, Pemba kwa miaka 34 mpaka umauti ulipomkuta. "Aliwaambia Wazanzibar 'nipo nanyi sasa hivi, ninawaahidi kuwa nitakuwa nanyi nikiwa ndani ya serikali au nje ya serikali. Nitakuwa nanyi nikiwa ndani ya chama na nje ya chama," alisema.

Zitto alisema Maalim Seif alikuwa na kifua kipana cha kutunza mambo mema na mabaya na aliweza kufanya maridhiano bila kikwazo.

"Ni mwanasiasa ambaye amefanya ama miafaka au maridhiano na kila Rais wa Zanzibar iliyoridhiana na Zanzibar yenye maridhiano kwa hakika, ni Zanzibar yenye maendeleo," alisema.

UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**INVITATION TO BID: NO. ITB/2021/SUP/001**
**FOR THE ESTABLISHMENT OF A FRAME AGREEMENT FOR THE SUPPLY OF JET A1 FUEL**

1. **Background**:

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers to submit firm offers for establishment of a frame agreement for the supply of Jet A1 Fuel

2. **Eligibility:**

Suppliers duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

**Kindly download the tender documents in the below link:**

**https://drive.google.com/drive/folders/1jHiwNjB5M9CCzg9uQlpJS24hTM4fkWtG?usp=sharing**

If you fail to access the link, please write to **ishobeza@unhcr.org** copy **ndassa@unhcr.org**

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Pre-bid Conference meeting will be held | Monday 03rd March 2021 |
| Deadline for receiving requests for clarification | Friday 15th March 2021 at 235900 hrs EAT |
| Deadline for submission of offers | Wednesday 30th March 2021 at 1600 hrs, EAT |

UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the

## HABARI KITAIFA

# TEC yatoa utaratibu mpya ibada, mikusanyiko

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), limetoa utaratibu mpya wa kushiriki ibada ndogo na kubwa za kanisa hilo, huku kukiwa na tahadhari kubwa ya maambukizi ya ugonjwa wa kushindwa kupumua.

Kwa mujibu wa kipeperushi cha TEC kilichothibitishwa na kusambazwa kwenye parokia, vigango na jumuiya za kanisa hilo kupitia Kurugenzi ya Mawasiliano yake ya baraza hilo, wametaka waumini kuelimishwa juu ya kujikinga.

Aidha, TEC imewaelekeza viongozi kuwaelimisha waumini mambo ya msingi ya kuzingatia na kuepuka kwa ajili ya kupambana na magonjwa hayo ya kuambukiza, ikiwamo kuzingatia usafi kwa kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na kutumia vitakasa mikono.

Pia waraka huo ulisema tayari kanisa limechukua hatua kadhaa za kupambana na magonjwa ya kuambukiza ikiwamo kufupisha muda wa ibada kwa kuongeza idadi ya misa, waumini kupokea ekaristi takatifu (sakramenti) kwa kutumia mikono, kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu wakati wa ibada.

Tahadhari zingine ni kuhakikisha watoa huduma kama mapadri, masista na makatekista wanajikinga, kusitishwa kwa maji ya baraka ya kuchotwa au kuchovya, kutopeana mkono wakati wa kutakiana amani.

Hatua nyingine ambayo imechukuliwa, kwa mujibu wa maagizo hayo, ni kutokushiriki jumuiya ndogo na misa kwa wanaojihisi kuumwa.

Waraka huo pia unawataka wanaohesabu sadaka kutumia vitakasa mikono, kujikinga kinywa kwa kitambaa safi au kiwiko cha mkono wakati wa kukohoa au kupiga chafya, kutokuchangia vipaza sauti wakati wa ibada, kutumia barakoa wakati wote na kutokuchangia vitabu vya sala.

Pia waraka unatoa maelekezo ya kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu, kutokumbatiana, kutobusiana, kutoshikana mikono, kutoshirikiana vyombo wakati wa kula na kunywa.

Kanisa hilo limewataka waumini wake kujifunza kuhusu magonjwa ya kuambukiza kupitia vyanzo sahihi na kuishinda hofu kwa kufuata maelekezo ya wataalamu na kuepuka kuonyesha upendo kwa wagonjwa.

# JPM kuongoza kuagwa Kijazi

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli leo anatarajiwa kuongoza waombolezaji kuaga mwili wa Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, katika viwanja vya Karimjee, Dar es Salaam.

Wakati mamia wakitarajiwa kuuaga mwili wake, taarifa zaidi zimebainisha kuwa kiongozi huyo anatarajiwa kuzikwa kesho nyumbani kwao, Korogwe mkoani Tanga.

Balozi Kijazi alifariki juzi katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini hapo, alikokuwa akipatiwa matibabu.

Akizungumza jana katika ibada ya kuaga mwili wa Balozi Kijazi kwenye eneo la hospitali hiyo, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Dk. Moses Kusiluka, alisema mwili huo umesafirishwa kwenda nyumbani kwake Mbweni, Dar es Salaam ambako utalala kabla ya kuagwa leo.

Alisema baada ya hapo, mwili wa marehemu utasafirishwa kwenda Korogwe kwa maziko.

"Sisi tuliofanya naye kazi kwa karibu kabisa ni vigumu kuamini ameondoka kwenye muda ambao hatukutarajia. Tunaomba Mungu tuuishi hata kwa kidogo wema wake maisha aliyoishi," alisema.

Akitoa salama kwa niaba ya mawaziri, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema alikuwa kiongozi mnyenyekevu ambaye aliwashauri mawaziri na kuwasaidia kuchambua vyema nyaraka walizokuwa wakiwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri.

Awali, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ambako marehemu alikuwa Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Faustine Bee, alisema mwezi huu Balozi Kijazi aliahidi kufanya ziara kwenye kila ndaki ya chuo ili kuzungumza na wafanyakazi na kuona huduma za kitaaluma zinavyotolewa.

"Kwa muda mfupi ambao tumekaa na kiongozi wetu tumejifunza mengi, ni mtu anayesikiliza, kushauri, kuelekeza na ambaye alitamani chuo kipige hatua mbele zaidi," alisema.

Prof. Bee alisema kwa chuo ni pigo kubwa ambapo kimepoteza wakuu wake wa chuo wawili kwa kipindi kifupi ambapo mtangulizi wake alikuwa ni Hayati Benjamin Mkapa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Alphonce Chandika, alisema pamoja na wadhifa aliokuwa nao, lakini alikuwa msikivu na kusikiliza ushauri wa madaktari kwa kipindi chote alicholazwa.

**WENGI WAMLILIA**

VIONGOZI, mabalozi na watu mbalimbali, wamemlilia Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, huku kila mmoja akimwelezea alivyokuwa mnyenyekevu, asiyejikweza, aliyejali watu wa kawaida na kuwa mstari wa mbele kutatua shida zao.

Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu, katika ukurasa wake wa twiter jana, alindika: "Nimepokea kwa masikitiko na mshtuko taarifa ya kifo cha Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, kilichotokea Februari 17, mwaka huu.

Naye Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliandika: "Nimepata taarifa za kifo cha Katibu Mkuu Kiongozi, pole kwa Rais John Magufuli na serikali nzima."

Katika ukurasa wake wa Twiter wa aliyewahi kuwa waziri katika wizara mbalimbali ikiwamo ya Maji chini ya Rais Jakaya Kikwete, Prof. Mark Mwandosya, aliandika: "Kwaheri Balozi Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi na aliyekuwa mwanafunzi Idara ya Sayansi ya Uhandisi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Balozi wa Tanzania nchini India, alinitembelea nilipolazwa Hospitali ya Apollo, mtu muungwana."

Nao Ubalozi wa India nchini, waliandika: "Kwa masikitiko makubwa tumesikitishwa na kifo cha Katibu Mkuu Kiongozi, alikuwa na makubwa ya kujivunia kama Balozi wa Tanzania nchini India. Mchango wake madhubuti katika kuimarisha ushirikiano baina ya nchi mbili, maombi yetu ni kwa familia yake."

- **Imeandikwa na Augusta Njoji, DODOMA, na Salome Kitomari, DAR**



Haijawahi kuwa rahisi hivi

CRDB BANK
Tunakusikiliza

# TAKUKURU yarejesha mamilioni mikopo umiza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, imeokoa Sh. milioni 176.5 zinazotokana na mikopo umiza kwa walimu wastaafu 16 na muuguzi zilizokuwa zimechukuliwa na Kampuni ya Geneva Credit Shop ya mjini Kondoa.

Fedha hizo zimerejeshwa kwa walimu hao baada ya TAKUKURU kumkamata mmiliki wa kampuni hiyo, Abubakary Kinyuma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema uchunguzi wa taasisi hiyo umebaini baadhi ya watumishi wa umma wilayani Kondoa wanapokaribia kustaafu, wamekuwa wakichukua mikopo midogo kwa kampuni hiyo na kuacha kadi zao za benki.

Kibwengo alisema kadi hizo huhifadhiwa hadi mafao yanapotoka ndipo kampuni hujitwalia fedha kwa riba kubwa hadi kufikia asilimia 10,000 kutoka kwa wakopaji hao.

"Kuna mwalimu mstaafu alikopeshwa Sh. 350,000, lakini pamoja na kurejesha Sh. milioni 4.6, bado alipokonywa nyumba yenye thamani ya Sh. milioni 37 iliyopo Kitalu C eneo la Ndachi East jijini hapa," alisema.

Alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato (TRA) wanaendelea kufuatilia kiasi cha kodi ambacho kampuni hiyo ya ukopeshwaji inadaiwa na TRA na wanafuatilia kiasi kingine cha fedha Sh. milioni 184.5 ambazo kampuni hiyo imezichukua kwa wakopaji 22.

Aliwasihi wakopeshaji fedha mkoani Dodoma kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi kuhusu mikopo na kuwataka kuacha tabia ya kuwaumiza wananchi kwa kuwatoza riba kubwa.

Katika hatua nyingine, TAKUKURU imerejesha Sh. milioni 51.6 kwa Chama cha Akiba na Mikopo cha Ufundi baada ya kuwabana wadaiwa sugu wa chama hicho. Alisema TAKUKURU pia imemrejeshea mfanyabiashara Dismas Kweka Sh. milioni tano kutoka kwa Richard Mwambeje, aliyeuziwa kiwanja namba 18 kilichoko Mbwanga jijini hapa kinyume cha utaratibu.

"Kiwanja hicho kilitolewa na mwananchi mmoja kama sadaka kwa Jumuiya ya Uamsho wa Wakristo Tanzania (UWATA), lakini Mwambeje aliyekuwa Katibu wa UWATA alikiuza kwa kutumia mkataba wa kughushi," alisema.

Mwalimu mstaafu, Juma Hindo, alishukuru taasisi hiyo kwa kuwasaidia kupata fedha zake ambazo alikuwa amekata tamaa kuzipata.

"Nikiwa kazini mwaka 2014, nilikopa Sh. 200,000 na baadaye nilibaini kampuni hiyo imechukua fedha nyingi kutoka benki kupitia kadi yangu," alisema Hindo.




Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo (kushoto), akionyesha fedha zaidi ya Sh. milioni 176.5 za walimu wastaafu, jijini humo jana, zilizorejeshwa na kampuni ya Geneve Credit Shop inayotoa mikopo umiza. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Familia yatoa masharti maziko ya Jaji

**Na Mwandishi Wetu**

FAMILIA ya Jaji (mstaafu) Raymond Mwaikasu imetoa masharti kwa waombolezaji ambao watapenda kwenda kwenye msiba wa baba yao.

Ilitoa masharti hayo ilipotangaza kifo cha baba yao, Jaji Mwaikasu aliyefariki dunia juzi baada ya kuugua kwa muda mfupi.

"Familia ya Jaji mstaafu Raymond Mwaikasu kwa masikitiko makubwa inakuarifu kutokea kwa msiba wa mpendwa baba yetu, Mzee Mwaikasu, kilichotokea katika Hospitali ya JKCI (Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete) baada ya kuugua kwa muda mfupi. Mipango ya mazishi inaendelea nyumbani kwake, Tabata Segerea.

"Tunatarajia kuupumzisha mwili wa baba yetu pale pale nyumbani Segerea siku ya Jumanne ijayo. Hata hivyo, kutokana na hali inayoendelea hivi sasa duniani kote, familia inaomba mkusanyiko rasmi wa msiba wa baba yetu uwe siku hiyo hiyo ya maziko tu," ilisema taarifa hiyo.

Taarifa ilisema watakaopenda kushiriki kuifariji familia kabla na siku ya maziko, wachukue tahadhari ya kujilinda na kuwalinda wengine kwa kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka au vitakasa mikono.

Pia iliwataka watakaokuwapo siku ya maziko wazingatie umbali kutoka mtu mmoja hadi mwingine na iwapo mtu atahisi hali yake ya kiafya si nzuri, basi asishiriki kwenye shughuli hiyo.

**PIGO KKKT**

Wakati familia hiyo ikitoa masharti hayo, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limepata pigo kwa kupoteza watumishi wake waandamizi wawili.

Taarifa kutoka katika taasisi tofauti za kanisa hilo ziliwataja watumishi hao kuwa ni pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa (SEKOMU), Prof. Vicent Kihiyo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Chuo hicho, Askofu Mteule wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Mchungaji Dk. Msafiri Mbilu, Prof. Kihiyo alifariki dunia jana asubuhi katika Zahanati ya Mount Usambara iliyoko Lushoto, Tanga, alipokuwa akitibiwa.

"Mazishi yatafanyika Jumamosi Februari 20 katika Kijiji cha Mhelo, Irente, saa 7:00 mchana,"alisema Dk. Mbilu.

Mbali na Prof. Kihiyo, mwingine aliyefariki dunia ni Msaidizi wa Askofu wa KKKT Dayosisi ya Ruvuma, Mchungaji Laurent Ng'umbi. Mchungaji Ng'umbi alifariki dunia Jumanne katika Hospitali ya Peramiho, Songea, alikokuwa akipatiwa matibabu.

# Silaha ya Nape iliyoibwa Dar yanaswa jijini Mbeya

**Na Romana Mallya**

SILAHA ya Mbunge wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, iliyoibiwa na watu wasiojulikana nyumbani kwake Kawe Beach jijini Dar es Salaam wakati amelala, imepatikana mkoani Mbeya.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliyasema hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari na kubainisha wanamshikilia mtu mmoja kwa tuhuma hizo.

Kamanda Mambosasa alisema wizi huo ulitokea Jumatatu ya wiki hii alfajiri nyumbani kwa mbunge huyo na silaha hiyo kupatikana siku mbili baadaye. "Bastola hii ni aina ya Glock 17 yenye namba YX647, ilikuwa na risasi 14 ndani ya kasha lake. Imekamatwa kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi Dar es Salaam na mkoani Mbeya. Mtuhumiwa mmoja anashikiliwa kwa tuhuma za wizi wa silaha hii," alisema.

Katika tukio lingine, jeshi hilo limewaua watu wawili wanaodaiwa majambazi wakati wa majibizano ya risasi baina ya watu hao na polisi.

Kamanda Mambosasa alisema tukio hilo lilitokea jana eneo la Kimara Stop Over wakati watuhumiwa hao wa ujambazi wakidaiwa kutaka kufanya uhalifu kwenye duka la Wakala wa Benki na mitandao mingine ya simu.

HABARI KITAIFA

# TASAF yanusuru wanafunzi kukatisha masomo Kahama

**Na Marco Maduhu, KAHAMA**

WATOTO wa walengwa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) katika Kijiji cha Ntobo, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, wamebainisha namna fedha za mfuko huo zilivyosaidia kuokoa ndoto zao kielimu. Modesta Alphonce, mmoja wa watoto hao wa wanufaika wa TASAF anayesoma darasa saba katika Shule ya Msingi Wichamike, alisema jana kuwa kabla ya wazazi wake kuingia kwenye TASAF, alikuwa mtoro shuleni kutokana na kukosa mahitaji muhimu, zikiwamo sare na madaftari. Alisema kuwa baada ya kukosa mahitaji hayo ya shule ilibidi akae nyumbani, huku wakienda kulima kama vibarua kwenye mashamba ya watu binafsi na wazazi wake, ili wapate fedha ya chakula, sare za shule na mahitaji mengine.

"Nilikuwa nimeshakata tamaa kabisa ya kuendelea na masomo kutokana na nyumbani kwetu kuwa maskini na kushindwa kunitimizia mahitaji ya shule, huwezi kwenda shule bila kuvaa sare wala kuwa na madaftari," alisema Alphonce.

"Baada ya wazazi wangu kuingia kwenye mpango wa TASAF, maisha yalibadilika na sikuwa mtoro tena shuleni, na ufaulu pia ukaongezeka sababu sikuwa ninakosa masomo tena. Nimetoka kushika nafasi ya 40 na 20, sasa ninashika nafasi ya 10 darasani," alisifu. Emmanuel Sahani anayesoma darasa la sita katika shule hiyo, aliishukuru TASAF kuwarudisha tena shuleni watimize ndoto zao kwa kuwa sasa wanapata mahitaji muhimu ya shule.

Alisema kuwa alikuwa amekata tamaa na shule na alikuwa ameamua kuchunga ng'ombe, lakini kwa sasa anaendelea na masomo.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule hiyo, Restuta Respikius, alisema awali wanafunzi ambao wanatoka kwenye kaya maskini, walikuwa watoro shuleni na kutofanya vizuri darasani, lakini mambo yamebadilika baada ya wazazi wao kuingia kwenye mfumo wa TASAF.

# Dar, Morogoro kukosa masika

**Na Faustine Feliciane**

MIKOA ya Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Morogoro inatarajia kukosa mvua kubwa katika msimu wa masika.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) jana ilitoa utabiri wa mvua za masika zinazoanza mwanzoni mwa mwezi ujao na kumalizika Mei, mwaka huu.

Katika utabiri huo, mikoa ya Kanda ya Ziwa - Mwanza, Geita, Shinyanga, Mara, Kagera na Simiyu na ile ya kaskazini, yaani Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga, inatarajiwa kuwa na mvua za wastani mpaka kubwa huku Dar es Salaam, Pwani, visiwa vya Pemba na Unguja vikitarajiwa kupata mvua za wastani. Akizungunza jana wakati wa kutoa utabiri huo, Mkurugenzi wa Huduma za Hali ya Hewa wa TMA, Dk. Hamza Kabelwa, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. Agness Kijazi, alisema mamlaka husika zinapaswa kuchukua tahadhari katika mikoa inayotarajiwa kupata mvua kubwa.

Sambamba na hilo, wanahabari wameaswa kutoa taarifa sahihi za hali ya hewa kutoka TMA ili waelimishe na kuwapa taarifa wananchi.

"Tunatarajia mvua hizi kwa mikoa ya kaskazini mwa nchi, Arusha, Kilimanjaro na Tanga kuanza wiki ya kwanza ya Machi huku mikoa mingine tukitarajia kuanza wiki ya pili ya Machi," alisema Dk. Kabelwa.

Pia alisema wakulima katika mikoa itakayopata mvua kubwa wanapaswa kufuata ushauri wa wataalamu wa kilimo hususani maofisa ugani.

Dk. Kabelwa alisema katika mikoa itakayopata mvua nyingi, kuna uwezekano wa kutokea maafa na uharibifu wa miundombinu na mlipuko wa magonjwa.

"Tunawashauri wananchi na mamlaka husika kuchukua tahadhari. Wananchi wanapaswa kuhakikisha wanafyeka majani na kuteketeza mandhari ya wadudu wanaoeneza magonjwa ya mlipuko," alisema Dk. Kabelwa.

Kuhusu mvua zilizopita za vuli, Dk. Kabelwa alisema utabiri ulitimia kwa asilimia 91.3.

# Radi yaua watoto wanne

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WATOTO sita ambao ni wanafunzi wa shule za msingi wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wamekufa katika matukio tofauti likiwamo la watatu wa familia moja kufa kwa kupigwa radi wakati wakicheza na wenzao.

Akizungumza wakati wa maziko ya watoto hao, Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, alisema kuwa tukio hilo lilitokea juzi saa 11 jioni wakati watoto hao wakicheza nyumbani kwao na wenzao 11.

Alisema wakiwa wanaendelea na michezo ya kitoto, ghafla ilipiga radi na kuua watatu wa familia moja, kitendo kilichosababisha vilio na simanzi katika Kijiji cha Nkana lilipotokea tukio hilo.

Alisema baada ya tukio hilo, ofisi yake ilipokea taarifa nyingine ya matukio mawili kutoka katika Kijiji cha Nchenje za mwanafunzi mwingine kufa kwa kupigwa radi na watoto wengine wawili kufa kwa kugongwa na gari katika maeneo tofauti kijijini hapo juzi.

"Ndugu zangu ninawaasa muone matukio haya ni mapenzi ya Mungu, na mchukulie kuwa ni misiba kama ilivyo mingine, na msihusishe na imani za kishirikina, kitendo kitakacholeta mafarakano baina yenu kwa kumtafuta mchawi ni nani," alisema.

Kaimu Ofisa Elimu Wilaya ya Nkasi, Agnes Martin, aliwataja watoto wa familia moja waliokufa kwa kupigwa radi ni Macrida Mtepa (7), Rita Chiwalala (5), na Exsavery Chipamba, huku mwanafunzi Kwilasa Siri alipigwa radi Kijiji cha Nchenje.

Watoto waliokufa kwa kugongwa na magari ni Bonifas Sapi (8) na Debora Chalula(12) wakiwa wakazi wa Kijiji cha Nchenje na walikuwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Nchenje.


Tpb Bank
Grow with us




Bodi ya Wakurugenzi, Uongozi na Wafanyakazi wa Benki ya TPB tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, **Maalim Seif Sharif Hamad.**
Tunatoa salamu za pole kwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, **Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi**, familia, ndugu, marafiki na Watanzania wote, kutokana na kifo cha Kiongozi mzalendo na mpenda haki kwa nchi yake.

**Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amen.**

www.tpbbank.co.tz | info@tpbbank.co.tz, marketing@tpbbank.co.tz | facebook/tpbbank | 0787 669977

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maalim Seif aenziwe kwa mchango wake

**MWILI** wa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, ulizikwa jana jioni kijijini kwake Mtambwe Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kiongozi huyo ambaye alikuwa gwiji la siasa za Zanzibar, alifariki dunia juzi asubuhi wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam.

Kifo chake kimeyasikitisha makundi mengi katika jamii wakiwamo wanasiasa, wananchi wa kawaida, wanaharakati, mabalozi na wengineo. Vyombo vya habari vya ndani na vya kimataifa vimewanukuu watu mbalimbali wakimwelezea Maalim Seif kwa mambo mbalimbali aliyoyafanya wakati wa uhai wake wa miaka 77 duniani.

Kikubwa wamemwelezea kuwa alikuwa mtu jasiri na aliyesimama bila woga kutetea haki za watu ambao walionekana kuonewa au kunyimwa haki zao. Maalim Seif anaelezewa kuwa daima alisimamia kile alichokiamini, hakuchoka kuwasaidia kwa hali na mali ukiwamo ushauri wote waliohitaji msaada wake.

Kadhalika, anatajwa kuwa mpenda amani na maridhiano kwa ajili ya maslahi ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Hili linadhihirishwa na jinsi ambavyo aliweza kutuliza hali ya hewa mara kadhaa amani na usalama ilipoingia katika majaribu.

Lingine ni kwamba Maalim Seif alipenda sana maendeleo ya watu na Zanzibar kwa ujumla, kiasi kwamba mara zote alipogombea urais wa Zanzibar, alikuwa na ajenda zilizoonyesha kwamba alikuwa na nia ya dhati kuiletea Zanzibar maendeleo.

Hata katika hotuba yake ya kuapa kuwa makamu wa Kwanza wa Rais kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) mwaka huu, alitamka wazi kwamba atashirikiana na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuhakikisha wanaipaisha nchi kimaendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo na kutekeleza miradi kikubwa ya kimkakati.

Katika suala la amani, mshikamano na umoja wa kitaifa, tutaendelea kumkumbuka Maalim Seif kwa kulitilia mkazo suala hilo kwa vitendo kutokana na mara kadhaa kukubali kushiriki katika mazungumzo ya kupata muafaka wa kisiasa.

Itakumbukwa alivyokubali kushiriki mazungumzo yaliyoleta muafaka wa mwaka 1999 yaliyosimamiwa na Jumuiya ya Madola kati ya chama chake (CUF) na Chama Cha Mapinduzi (CCM) baada ya mvutano uliotokana na uchaguzi wa mwaka 1995.

Maalim Seif pia alikubali chama chake (CUF) kushiriki katika mazungumzo ya kusaka muafaka wa pili uliopatikana Machi, 2001, baada ya machafuko ya Januari 26 na 27, mwaka 2001 yaliyosababishwa na uchaguzi mkuu wa mwaka 2000.

Kiongozi huyo pia ndiye aliyeshirikina na aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Amani Abeid Karume, kuzungumza pamoja na kukubaliana kuwapo kwa maridhiano yaliyowezesha kubadilisha katiba ya Zanzibar kuruhusu kuwapo kwa SUK mwaka 2000.

Maalim Seif ameondoka duniani akiwa na ndoto za kuona Wazanzibari wakibaki kuwa wamoja, sisi kwa upande wetu tunawahimiza Wazanzibari wote kuweka kando tofauti za itikadi za kisiasa badala yake kuhakikisha wanabaki kuwa wamoja, na kushirikiana kupaisha uchumi wao kupitia rasilimali walizonazo ikiwamo bahari.

Tunaamini kwamba Rais Mwinyi atashauriana na Chama cha ACT-Wazalendo kupata mrithi wa Maalim Seif katika SUK, kwa lengo la kuendelea kutekeleza yale yote ambayo serikali hiyo iliwaahidi Wazanzibari. Hakika atakumbukwa na wengi kutokana na mambo mengi mema aliyoyafanya na kuyasimamia wakati wa uhai wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Zisidharauliwe fursa hizi za ajira, zichangamkiwe

Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya vijana jijini Dar es Salaam, wamejiajiri kwa kufanya kazi ya kukusanya taka kutoka katika nyumba za wakazi, wakitumia mikokoteni na kwenda kutupa kwenye maeneo mbalimbali.

Katika maeneo hayo, taka hizo hutupwa kandoo ya mito na kwenye vichaka, hali ambayo ni wazi kwamba inachangia kuchafua wa mazingira na wakati mwingine kuhatarisha afya za watu.

Ni kweli vijana hao wanajitafuta riziki kwa njia halali, lakini uhalali unaharibiwa na mtindo wa kutupa taka kwenye maeneo ambayo siyo rasmi, kwa kuwa ni hatari kwa afya zao pia na wanachafua mazingira.

Mto Ng'ombe eneo la Manzese Uzuri, ni moja ya ambayo wasomba taka hao walikuwa wakiyatumia, wamedhibitiwa, lakini inawezekana wakawa wametafuta mengine ili kuendeleza ajira yao hiyo.

Inaelezwa kuwa, wenye taka huwatumia hao kwa kuwa bei yao ndogo, kutokana na kwamba wakishasomba, wanajua wenyewe wanakwenda kutupa kando ya mto au vichakani ambako hawatozwi gharama yoyote.

Kwa hali kama hiyo, ni vyema kuwakumbusha wote kuanzia wenye taka na wazoaji, kwamba mtindo huo si mzuri, wazoaji wasifikirie fedha tu, pia walipaji wasiangalie unafuu wa kile wanachotoa.

Ikumbukwe kuwa taka huwa zinakusanywa pamoja kandokando ya barabara za mitaani na hata barabara kuu, ambako magari hufika na kuzichukua na kwenda kutupwa kwenye maeneo rasmi (dampo).

Wenye taka wakikubaliana na wazoaji na kuwalekeza kuzipeleka kwenye maeneo rasmi ya kukusanyia, hata kama gharama ya uzoaji itaongezeka, basi wailipe ili kuachana na mtindo wa kuchafua mazingira. Ikumbukwe kuwa, Jiji la Dar es Salaam kwa sasa lina mkakati wa kurejeleza taka ngumu ili kuhamasisha teknolojia zinazolenga uzalishaji na utumiaji wa bidhaa zitokanazo na taka rejea.

Katika kufanikisha hilo, Jiji linasema kutakuwapo na uhamasishaji wa jamii juu ya umuhimu wa kurejeleza taka, kwa kushirikiana na manispaa zake zote ili kuhakikisha utenganishaji wa taka unafanyika kuanzia ngazi za uzalishaji.

Hiyo inatokana na kile kinachoelezwa na jiji kuwa, urejelezaji wa taka una faida nyingi katika jamii, ikiwamo kuongeza thamani ya taka na kipato katika jamii, kupunguza marundo ya taka katika mitaa na maeneo ya jamii.

Vilevile, unasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa dampo, kupunguza gharama za udhibiti taka katika manispaa na kuongeza uelewa wa jamii katika uchambuzi wa taka kuanzia ngazi ya kaya.

Linatambua kuwa kuna ongezeko la aina tofauti za taka, kuanzia ngumu zikiwamo za viwandani, majumbani na hospitalini ambazo hutupwa maeneo mbalimbali na kusababisha uchafuzi wa mazingira.

Hivyo, mtindo wa kutupa taka maeneo yasiyo rasmi, unaweza kukwamisha mkakati wa jiji, kutokana na kwamba, wazoaji huzikusanya pamoja taka ngumu na taka maji na kwenda kutupa wanakojua wenyewe.

Wakati kukiwa na mkakati huo, ni vyema pia vijana wanaofanya ajira za kusomba taka kutoka katika majumba ya watu, sasa wazipeleke mahali sahihi kwa ajili ya kuchambuliwa na kufanyiwa urejelezaji.

Muungwana anaamini kuwa, mazingira yanayoandaliwa na jiji, yana umuhimu, hasa kutokana na kwamba yatawezesha ukuaji wa sekta ya urejeshaji taka ngumu na kuongeza viwanda na ubora wa bidhaa zake.

Hatua hiyo inaweza kusaidia kupata soko ndani na nje ya nchi na kukuza pato la jamii na taifa, hivyo ni vyema kuunga mkono, ili kuongeza ajira bila kuchafua mazingira kama ilivyo sasa kwenye baadhi ya maeneo.

Pia wananchi wa maisha ya chini wakiwamo vijana na wanawake wanaweza kushiriki katika ubunifu na utumiaji wa teknolojia za urejeleshaji taka na hatimaye kuboresha usafi.

Pamoja na hayo, mkakati wa jiji unaonyesha wazi kuwa taka ni mali, na zinaweza kuwafanya vijana wanazisomba kutoka majumbani mwa watu wakafaidika nazo badala ya kuzitupa ovyo na kuchafua mazingira.

Kwa kuwa Jiji linasema kuwa huo ni mwanzo wa kutambua na kurasimisha sekta ya urejeleshaji taka ambayo awali ilikuwa ikiendeshwa na taasisi binafsi na vikundi visivyokuwa rasmi, hivyo ni fursa ya kuchangamkiwa.

HABARI KITAIFA

# Kortini madai kumbaka mtoto wa miaka 12

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kata ya Mnazi Mmoja katika Manispaa ya Lindi, Mohamedi Issa (26) amefikishwa mahakamani kwa tuhuma za kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 12 (jina limehifadhiwa).

Issa alifikishwa juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya, Maria Batraine, na kusomewa mashtaka na Mwanasheria wa Serikali, Rabia Ramadhani. Mwanasheria huyo alidai kuwa Februari 7, mwaka huu, katika eneo la Mnazi Mmoja, mshtakiwa akiwa anafahamu anachokifanya ni kosa, alishiriki tendo la kimapenzi na mtoto huyo.

Alidai kwamba kutokana na kitendo hicho, mshtakiwa amefanya kosa chini ya vifungu 130 kifungu kidogo (1) na (2) (e) na 131 (1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 rejeo la mwaka 2019.

Hakimu Batraine alipomuuliza mshtakiwa kuwa alichosomewa amekielewa na kukikubali, alikiri kufanya tendo hilo, lakini alikataa umri wa mtoto huyo kuwa ni miaka 13 badala ya 12.

"Mheshimiwa Hakimu nakubali kushiriki kufanya naye mapenzi, lakini hapo kwenye umri hapana kwani aliniambia ana miaka 13 na siyo 12," alidai mshtakiwa.

Pia Hakimu alipomuuliza kwa nini aliamua kufanya tendo la ndoa na mtoto mwenye umri ambao kisheria hairuhusiwi, mshtakiwa alijibu kwa kudai kuwa shetani alimpitia wala halikuwa kusudio lake kufanya hivyo.

Hakimu Batraine baada ya kusikiliza na kuyaona mashtaka na majibu ya mshtakiwa, aliahirisha kesi hiyo hadi Machi 2, mwaka huu, kwa ajili ya kutoa uamuzi.

Mshtakiwa amepelewa rumande hadi tarehe hiyo baada ya kukosa wadhamini.

# Taasisi yahimiza utalii wa ndani kuongeza mapato

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Global Education Link (GEL) kupitia mpango wa Education Tourism imeendelea kuwapeleka wanafunzi wa shule na vyuo maeneo mbalimbali ya kihistoria na utalii nchini kama sehemu ya kuwajengea utamaduni wa kutembelea maeneo hayo ili kuliingizia taifa mapato.

Mkurugenzi Mkuu wa GEL, Abdulumalik Mollel, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wanafunzi wanaotarajia kwenda kusoma nje ya nchi kupitia taasisi yake ambao walitembezwa maeneo mbalimbali ya kihistoria ili kujifunza kwa vitendo.

GEL ni taasisi inayowaunganisha wanafunzi wa Tanzania na vyuo vya nje ya nchi na pia wanafunzi wa nje ya nchi ambao wanataka kusoma kwenye vyuo vya hapa nchini.

Mollel alisema badala ya kutegemea watalii kutoka nje ya nchi pekee, kuna haja ya kuwaandaa Watanzania kuwa na utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii na maeneo ya kihistoria yanayopatikana nchini tangu wakiwa wadogo ili kuwajengea shauku ya kuendelea kuvitembelea hata wakiwa watu wazima.

Alisema taasisi yake imeshapeleka zaidi ya wanafunzi 3,000 wa shule na vyuo vikuu maeneo mbalimbali ya kihistoria nchini ili kujifunza historia na utajiri wa vitu mbalimbali vinavyopatikana nchini.

Mollel alisema Tanzania si nchi maskini kama Rais John Magufuli anavyosisitiza kwa kuwa imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi kama mbuga za wanyama na maeneo ya kihistoria. Alisema kama Watanzania watayatembelea na kulipia kiasi kidogo cha pesa, taifa litaingiza fedha nyingi.

"Tuna maeneo mengi ya kihistoria ambayo Watanzania hawayajui. Sasa sisi Global kupitia 'Education Tourism' tunataka kuwaelimisha Watanzania kuhusu maeneo haya wayatembelee kwa sababu kwa wenzetu maeneo kama haya yanawaingizia fedha nyingi," alisema Mollel.

"Mheshimiwa Rais amesisitiza umuhimu wa kufundishwa somo la historia ya Tanzania. Ni kweli kabisa kuna umuhimu huo kwa sababu kuna vitu vingi tunavyo, lakini ni watu wachache wanaovijua. Mfano tuna wanyama lakini hatujui sifa zao. Mnyama kama tembo inabidi mtu ajue sifa zake kuanzia anavyozaa, anaishi miaka mingapi, tabia zake mbugani badala ya kuishia kumwona kwenye TV au mbugani," alisisitiza Mollel.

Alitoa mfano kuwa iwapo Watanzania watahamasika na kuchangamkia kutembelea vivutio vya utalii na maeneo ya kihistoria nchini, pato la taifa litaongezeka maradufu na kwamba taasisi yake imejipanga kuhakikisha Watanzania wanaamka na kuvithamini vivutio vilivyopo.

"Tukipata Watanzania milioni 10 tu wanaotembelea vivutio vya utalii kila mwaka, tutapata mabilioni ya fedha kwa sababu maeneo ya kihistoria na utalii ni mengi sana. Badala ya kila sikukuu kwenda ufukweni, watu waelimishwe kwamba kuna maeneo mengine mazuri tu ambayo hawajawahi kufika waende wakayaone," alisema.

Alisema GEL kwa muda mrefu imekuwa ikiwajengea utamaduni huo vijana wa kitanzania kwani kabla ya kusafiri kwenda nje ya nchi kimasomo wamekuwa wakiwatembeza kwenye maeneo ya utalii na ya kihistoria na kuwataka wakayatangaze wakiwa nje ya nchi.

"Tunawakutanisha wanafunzi na wataalamu waliobobea kwenye fani mbalimbali wanawaelimisha kuhusu fani hizo na wao wanapata nafasi ya kuuliza maswali sasa hii inakaa kichwani kwa mwanafunzi na hapo ndipo wanaanza kujenga mapenzi na fani wanazotaka," alisema.


Tpb Bank
Grow with us




Bodi ya Wakurugenzi, Uongozi na Wafanyakazi wa Benki ya TPB tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha **Mhe. Balozi John William Kijazi,** Katibu Mkuu Kiongozi

Tunatoa salamu za pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dk. John Pombe Magufuli**, familia, ndugu, marafiki na Watanzania wote.

**Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amen.**

www.tpbbank.co.tz ‖ info@tpbbank.co.tz, marketing@tpbbank.co.tz ‖ facebook/tpbbank ‖ 0787 669977

HABARI KITAIFA

# Waziri achimba mkwara wanaokwamisha kukamilika kiwanda cha sukari Mkulazi

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imewaonya wenye viwanda vya sukari wanaofanya jitihada za kukwamisha uanzishwaji wa kiwanda cha sukari cha Mkulazi II kilichoko Kilosa mkoani Morogoro.

Onyo hilo lilitolewa na Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alipotembelea kiwanda hicho na kusikiliza kero za wakulima wa miwa kutoka vijiji vya Msowero, Malangali, Mvumi, Wami na Mbigiri.

Miongoni mwa kero zilizowasilishwa na wakulima hao ni pamoja na kuchelewa kukamilika kwa kiwanda hicho takribani miaka mitatu, hivyo kusababisha waliolima miwa yao na kukosa soko, kufilisika kutokana na mikopo waliochukua kwenye Benki ya Azania.

Prof. Mkenda alisema anazo taarifa kuna baadhi ya watu wakiwamo wamiliki wa viwanda vya sukari wanafanya jitihada za kuzuia kiwanda cha Mkulazi II kufanya kazi.

Kutokana na taarifa hizo, alisema watu hao wanapoteza muda wao bure na serikali itapambana na kuhakikisha kiwanda hicho kinafanya kazi.

"Naomba niwashukuru wakulima kwa uvumilivu mpaka hapo tulipofika na changamoto nyingi, lakini nawahakikishia ninazo taarifa sasa kiwanda hapa kitakamilika na kitaanza kazi," alisema.

"Na sisi wote tutasimama nao na zile changamoto ambazo zingine hawajazisema tutapambana nazo. Anayezuia kiwanda hiki kufanya kazi tutampasua tunajua nini kinaendelea tunapambana na mambo mengi sana hiki kiwanda kitaanza kazi," alisisitiza.

Prof. Mkenda alisema viwanda vya sukari vya Kilombero na Mtibwa vianze kujitathimini kutokana na kushindwa kununua miwa yote ya wakulima wa nje kutokana uwezo mdogo wa uchakataji huku serikali ikiwapa vibali vya kuagiza sukari kutoka nje ili kuziba pengo linalojitokeza.

"Tuna maslahi kama serikali kuhakikisha tunajitosheleza kwa sukari. Kama maslahi yetu katika soko la sukari yanalandana na maslahi mapana ya mkulima wa miwa ni kupata soko na serikali kujitegemea kwenye sukari," alisema.

Alisema kiwanda kikubwa zaidi cha sukari nchini ni Kilombero kulinganisha na vingine kikiwamo cha TPC mkoani Kilimanjaro ambavyo vyote serikali ina hisa ya asilimia 25, lakini TPC inachangia fedha nyingi serikalini kuliko cha Kilombero ambacho ndicho kikubwa.

"TPC ni kidogo kuliko Kilombero, lakini wamewekeza katika miundombinu ya umwagiliaji na mbegu bora na kwa hekta moja wanapata tani 160 za miwa wakati Kilombero wanapata tani 80 kwa hekta. Sisi wizara na wakulima wetu wa miwa tunataka uwekezaji kama wa TPC," alisema.

Mbunge wa Mikumi, Dennis Londo, akizungumza kwa niaba ya Mbunge wa Kilosa, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema pamoja na wakulima kuhamasika kulima miwa, hawana uhakika wa soko kwa kipindi cha miaka mitatu.

Alisema uhakika huo unatokana na kucheleweshwaji wa ukamilishwaji wa kiwanda cha Mkulazi II na matokeo yake miwa yao kwenda kuuzwa kwa bei ya Sh. 60,000 mpaka 65,000 kwa tani kulinganishwa na gharama za uzalishaji.

# Waajiri waonywa kubadilisha vyeo watumishi bila kufuata utaratibu

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewataka waajiri kutowabadilishia vyeo vya kimuundo maofisa tarafa na watendaji kata walioajiriwa mwaka 2018 wakiwa na taaluma mbalimbali kwa lengo la kuziba nafasi zilizoachwa wazi na watumishi waliostaafu na walioondolewa baada ya kubainika kuwa na vyeti vya kughushi.

Ndejembi alitoa maagizo hayo juzi, mkoani Iringa wakati akizungumza na wakuu wa idara na taasisi mbalimbali mkoani humo.

Ndejembi alisema wako baadhi ya waajiri wamewabadilishia watumishi hao vyeo vya kimuundo bila kibali cha Katibu Mkuu Utumishi ambaye ndiye mwenye mamlaka na alishatoa maelekezo ya kutowabadilishia kada wala kuwahamisha vituo vya kazi mpaka watakapotimiza miaka mitano.

"Watumishi hao wakati wa kuajiriwa, walitia saini mikataba ya kutumikia vyeo vyao bila kubadilisha wala kuhama mpaka watakapotimiza miaka mitano, hivyo waajiri kama mna upungufu wa watumishi ambao wana sifa walizo nazo watumishi hao, ombeni kibali kwa Katibu Mkuu Utumishi ili mpatiwe watumishi mbadala," alisema.

Pia alisema suala la watumishi wa umma kukaimu nafasi za uongozi kwa muda mrefu inatokana na baadhi ya waajiri kuwakaimisha bila kuwa na kibali cha Katibu Mkuu Utumishi.

Alifafanua kuwa zaidi ya asilimia 60 ya wanaokaimu hawana sifa za kutumikia vyeo walivyokaimishwa, hivyo wanapoteza sifa za kupata kibali cha Katibu Mkuu Utumishi na stahiki husika.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka waajiri kuwaombea vibali kwa wakati kwa Katibu Mkuu Utumishi watumishi ambao wana sifa za kukaimu ili wapate uhalali wa kutumikia vyeo walivyokaimishwa na kupata stahiki husika.

Ndejembi alifanya ziara ya kikazi mkoani Iringa yenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa wakuu wa idara na taasisi za umma mkoani humo.




## Shukrani

Familia ya **Marehemu Ndugu Harith Bakari Mwapachu** inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Prof. Mabula Nchembe Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Mkuu wa Kitengo cha Muhimbili Emergency, Dkt. Juma Mfinanga, Madaktari bingwa Muhimbili, Dkt. Sensa na Dkt. Pazi, Madaktari bingwa wa Jakaya Kikwete Cardiac Institute, Prof. Janabi na Dkt. Shemu, Daktari wa hospitali ya TMJ, Dkt. Dossaji na Daktari Mkuu wa HCG Bangalore, India, Dkt. Sridhar.

Aidha familia inawashukuru pia Mkuu wa Mkoa Tanga, Mheshimiwa Martin Shigela, Mkuu wa Wilaya ya Tanga mjini, Mheshimiwa Thobias Mwilapwa, wanachama wa CCM Tanga pamoja na viongozi wa dini.

Tunawashukuru ndugu, jamaa, marafiki na majirani wote kwa ushirikiano, huduma na michango yao ya hali na mali.

**Inna lillahi waina ilahi rajiun**

# TMA: Tumieni taarifa kukabili tabianchi

**Na Maulid Mmbaga**

KUTOKANA na matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii na kuhusisha tabianchini, wadau wa hali ya hewa kutoka sekta mbalimbali wametakiwa kutumia taarifa za hali ya hewa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Hayo yalisema jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Burhani Nyenzi, wakati akifungua mkutano wa wadau wa utabiri wa mvua za msimu wa masika, uliofanyika Dar es Salaam.

Nyenzi aliwasihi wadau wote wa hali ya hewa katika sekta mbalimbali kujihusisha zaidi katika kuelewa na kufuatilia masuala ya hali ya hewa na mabadiliko yake ili kuchukua hatua za kujikinga na kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema kwa kufanya hivyo, watasababisha mazingira wanayoishi yaendelee kubaki salama na kuwa katika asili yake na yenye kuvutia kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kwa kizazi hiki na vizazi vijavyo.

Pia ni jukumu la kila mtu kuendelea kuelimishwa kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa na namna ya kukabiliana nayo na wakati huo huo wakiendelea kutekeleza sera na mikakati ambayo itasaidia kutumia vyema huduma za hali ya hewa katika kuinua uchumi wa nchi.

"Mabadiliko ya tabia nchi ni halisi. Tumeshuhudia athari mbalimbali zinazotokana na mabadiliko haya ikiwa ni pamoja na kuwa na vipindi vya mvua kubwa, kubadilika kwa misimu ya mvua hasa tarehe za kuanza na kuisha kwa mvua, wote tumeshuhudia mvua zilizo nje ya msimu kwa mwaka huu wa 2021.

"Mvua zilinyesha katika maeneo ambayo kwa kawaida huwa ni makavu kwa miezi ya Januari na Februari, hali hii inasababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa," alisema Nyenzi.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Dk. Agnes Kijazi, alisema mkutano huo unalenga kujadiliana na kupata maoni ya wadau juu jinsi utabiri wa mvua za masika utakavyoweza kutumika kwa tija katika sekta mbalimbali hapa nchini na hivyo kuendeleza na kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa na matumizi yake kwa jamii.

Alisema kuna haja ya kutambua uwezo wa utabiri wa hali ya hewa na husan utabiri wa msimu kama zana yenye nguvu katika kusaidia watoa uamuzi kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

Kijazi alibainisha kuwa kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Tumia Taarifa za Utabiri Kukabiliana na Changamoto za Mabadiliko ya Hali ya Hewa'.

Mdau kutoka Wizara ya Kilimo, Robert Dimoso, alisema katika kipindi cha msimu wa mvua za vuli ulioanza Oktoba mpaka Desemba, mwaka jana, maeneo mengi yalipata mvua za chini ya wastani, hivyo kusababisha kupata unyevunyevu mzuri kwenye udongo ambao ulisaidia kustawi vizuri kwa mazao.

"Kuna maeneo machache yalipata mvua za juu ya wastani hasa mikoa ya Kanda ya Ziwa ambayo ilichangia kuharibika kwa maharage, lakini kwa ujumla utabiri uliendana na uhalisia kama ulivyotabiriwa," alisema Dimoso.



Mnufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa kunusuru Kaya Maskini (TASAF), Fotunata Mosha, mkazi wa Iselamagazi, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, akionyesha kondoo 26 ambao amewapata kupitia fedha za ruzuku kutoka mfuko huo, na kumtoa kwenye umaskini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Kampuni ununuzi tumbaku zaonywa kuajiri watoto

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KAMPUNI za kununua zao la tumbaku zimepigwa marufuku utumikishwaji wa watoto katika mashamba ya tumbaku, ili wanafunzi hao watumie muda huo kwenda shule.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Kampuni ya Alliance one, David Mayunga, alipokuwa akitoa taarifa ya Kampuni hiyo katika mkutano mkuu wa 25 wa Chama Kikuu cha Ushirika wilayani Kahama (KACU).

Mayunga alisema kitendo cha wakulima kuwatumikisha watoto katika mashamba yao hakikubaliki kwa kuwa muda huo wanapaswa kwenda shule ili kutimiza ndoto zao.

Alisema wakulima ambao wako chini ya Kampuni ya Alliance one, wasithubutu kuwatumikisha watoto kwa kuwa ikibainika wanafanya hivyo, tumbaku wanayozalisha haitanunuliwa.

Mkurugenzi huyo aliwahimiza wakulima wa zao hilo kuhakikisha wanapanda miti katika maeneo yao ya kilimo hekari moja kwa miti 600 ili kulinda mazingira katika maeneo hayo.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wilayani Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, alisema chama hicho kiko mbioni kupata ekari 2,000 kwa ajili kupanda miti katika maeneo mbalimbali ya wakulima wa tumbaku hususani katika Halmashauri ya Ushetu.

Alisema lengo la ushirika huo ni kuhakikisha unakuwa na mashamba miti katika halmashauri zao na kuongeza kuwa kila chama cha msingi kinatakiwa kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya ununuzi wa maeneo hayo kwa ajili ya kupanda miti.

## Equity yaingia ubia kimataifa

**Na Beatrice Shayo**

BENKI ya Equity (T) imetangaza ubia na kampuni kinara katika tasnia ya huduma za fedha duniani kwa ajili ya kurahisisha upokeaji na utumaji wa fedha kwa lengo la kuongeza tija katika huduma hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa za Benki ya Dunia za mwaka 2019, Tanzania inakisiwa kuwa na takriban wananchi milioni nne wanaoishi ughaibuni. Kwa mwaka, wananchi hao hutuma nyumbani zaidi ya dola za Kimarekani milioni 437.

Akizungumza katika uzunduzi wa huduma hizo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Equity, Robert Kiboti, alisema huduma hizi zipo katika vipengele viwili, cha kwanza ni huduma za upokeaji na utumaji fedha nje ya nchi.

Alisema Benki ya Equity inashirikiana na kampuni kubwa za World Remmit, Western Union, Money Gram, Small World, SimbaPay, Transact, Terrapy and Thunes ili kutuma na kupokea fedha kwa nchi zaidi ya 250 duniani.

"Huduma ya pili ni ya mfumo maalum wa ndani ujulikanao kama "Inter country transfer" ambao unawezesha wateja wa Benki ya Equity kutuma fedha kwenda kwenye mtandao wa matawi yote ya Benki ya Equity katika nchi za Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Congo, na Sudani Kusini kwa gharama nafuu ya kiasi cha shilingi 10,000 kwa muamala usiozidi kiasi cha shilingi milioni kumi," alisema.

Aliongeza: "Tunafuraha kubwa kuzindua rasmi huduma hizi zenye lengo la kuwaunganisha Watanzania waliopo nje ya nchi na familia zao hapa nyumbani. Tumejiwekea lengo la kutanua wigo wetu katika mtandao huu ili kuwafikia Watanzania wote nje ya nchi kwa asilimia 100."

Kiboti alisema kuungana katika kampuni hizo kubwa katika tasnia ya kutuma na kupokea fedha kama World Remits, Western Union kutawapa uwezo wa kufika kila kona ya dunia na kufikisha huduma zao.

## Takukuru yakosoa viongozi ushirika

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

IMEELEZWA kuwa baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika nchini wamekuwa ni wagumu katika kukabidhi madaraka muda wao wa uongozi unapopita kutokana wengi wao kuwa na madeni makubwa.

Hayo yalibainishwa juzi na Kaimu Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Kahama, Frank Masilange, juzi wakati akitoa salamu za taasisi hiyo katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa 25 wa Chama cha Ushirika cha wilaya hiyo (KACU).

Masilange alisema TAKUKURU inaangalia taratibu zote za kifedha katika eneo husika zinavyofanyika katika kipindi kizima cha uongozi wa watumishi wa ushirika ili kuhakikisha kuwa wanakabidhi mikoba yao salama muda wao unapokuwa umemalizika.

"Kuna baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika nchini wamekuwa wagumu wa kukabidhi madaraka vipindi vyao vya kuongoza vinapokuwa vimeisha kutokana na hali ngumu ya kuwa na mrundikano mkubwa wa madeni kutoka sehemu mbalimbali pamoja na wakulima," alisema Masilange.

Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Albet Msovela, liyekuwa mgeni rasmi katika mkutano huo akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, alikipongeza chama hicho kwa kufanya vizuri katika kipindi hiki ikiwamo kurejesha madeni yote iliyokuwa ikidaiwa na baadhi ya taasisi za fedha

# Madiwani waingia kazini kukusanya mapato

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MADIWANI wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani ambao ni wajumbe wa kamati ya fedha, wameamua kukaa katika stendi ya mabasi kufuatilia magari yanayoingia na kutoka, lengo likiwa ni kujiridhisha na mapato halisi yanayokusanywa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapa, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Musa Ndoma, alisema madiwani hao watatumia wiki moja saa 24 kukaa stendi na barabarani, wiki nyingine watakuwa katika machimbo ya mchanga. Ndomba alisema wameamua kufanya hivyo kujiridhisha na mapato yanayokusanywa kujua pia ni kiasi gani kimekuwa kinapotea.

Alisema katika wiki ambayo watakuwa stendi ya mabasi watakaa hapo hadi saa tatu usiku na kuanzia saa nne watahamia nje barabara kuu Chalinze Morogoro kupata idadi kamili ya mabasi ambayo hayaingii stendi majira ya usiku.

" Wanaochukua ushuru wanakaa stendi hadi saa tatu usiku, lakini yapo mabasi ambayo yanapita saa nne hayaingii stendi kwa hiyo muda wa kukaa ndani ya stend ukipita madiwani watahamia nje," alisema na kuongeza:

"Tunataka kujua tunapoteza kiasi gani kwa mabasi ambayo hayaingii stendi, baada ya kupata takwimu halisi stendi na kwenye mchanga maazimio yetu tutayatoa kikao cha baraza," alisema Ndomba. Katika hatua nyingine alisema ili kukabiliana na mashamba pori katika mji huo kila diwani kupitia vikao atawasilisha idadi ya mashamba pori ambayo hayajaendelezwa kwenye eneo lake ili hatua za kisheria zichukuliwe.

Alisema baada ya kujiridhisha na taarifa za maeneo ambayo hayajaendelezwa kwa muda mrefu, yapo ambayo yatagawiwa kwenye Taasisi yatumike kwa ajili ya shule au Zahanati.

"Zipo baadhi ya kata hazina shule wala zahanati na kuna watu wamechukua maeneo kwa muda hawayaendelezi ...tunataka tuyachukue yarudi serikalini kwa kufuata taratibu, tutaomba yaendelezwe na taasisi zenye kuhitaji," alisema.

Alitoa wito kwa watu binafsi ambao pia wamechukua maeneo na wameendelea kuyaacha kuwa mapori hadi sasa wayaendeleze kabla hayachukuliwa na Serikali.




Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard (wa pili kulia) akipeana mkono na Waziri wa Kilimo, Maliasili na Umwagiliaji Zanzibar, Soud Nahoda Hassan, wakati wa makabidhiano ya vifaa vya ujenzi vikiwamo mabati mia mbili kutoka benki ya NMB kwa ajili ya shule ya Jambiani Sekondari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashimo yasiyotumika uchimbaji yafukiwa

**Na Mohab Dominick ,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika mgodi mdogo wa Mwime namba mbili katika Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, wameanza kuitikia maagizo kutoka katika ofisi ya madini kwa kufukia mashimo yaliyopo katika eneo hilo ambayo yameachwa bila kufanyika shughuli za kiuchimbaji.

Ofisa Uhusiano na Mawasiliano wa Mgodi huo, Christopher Bundala alisema: "Tumeanza rasmi kuyafukia mashimo ambayo kimsingi hayafanyi kazi, hivyo kuhatarisha maisha ya watu na tumefikia asimilia 90, ingawa kuna changamoto nyingi zinazokabili suala hilo."

Akizungumza na waandishi wa habari, Bundala alisema kufukiwa kwa mashimo hayo ambayo yalibaki kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo wahusika kuishiwa mitaji na pia kutaepusha ajali ambazo zinaweza kutokea na kusababisha madhara kwa watu. Alisema kuna mashimo mengine yamechimbwa na kufikia mita 80, hali ambayo katika zoezi la kuyafukia kunahitaji rasilimali fedha ikiwamo muda ili kuyafukia, hivyo kuepusha majanga yasiokuwa ya lazima kutokea kama vile watu kufukiwa.

Bundala alisema kazi hiyo wanaifanya kwa thadhari kubwa kwa kufuata agizo kutoka katika ofisi ya madini, ikiwamo kuyazia alama mashimo hayo, huku akiongeza kuwa kwa kufanya hivyo, watu watakuwa na tahadhari kubwa.

Alisema wakaguzi katika mgodi huo wamekuwa wakitoa elimu kila siku kwa ajili ya kujikinga majanga ambayo yanaweza kusababishwa na mashimo hayo, yalikuwa mengi na sasa yameachwa bila ya kuwa na wenyewe. Bundala akizungumzia kuhusu wavamizi wa mashimo, alisema wamejipanga kuhakikisha kuwa wavamizi hao wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo husika vya kisheria, kwani uhalifu huo ni kama mwingine, na kwamba wanaweza kuhukumiwa kama sheria inavyosema. Katika hatua nyingine, alisema wameshajenga vyoo katika eneo hilo na kuongeza kuwa walioopo kwa sasa ni wale ambao wanaoingia na kutoka, hali ambayo ni rahisi katika kuhakikisha wanatunza mazingira vizuri ya maeno hayo.

Kamishina wa Madini Mkoa wa Madini Kahama, Ernest Maganga, alisema mgodi wa mwime na maeneo mbalimbali ya uchimbaji wadogo wameshatoa maelekezo kwa viongozi wa migodi yote katika kipindi hiki cha mvua kuhakikisha maeneo hayo yapo salama,

# Shule yapigwa jeki mabati 200

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB Tawi la Zanzibar imekabidhi mabati 200 na vifaa vyengine vya ujenzi kwa ajili ya ukarabati wa vyumba vya madarasa ya Shule ya Sekondari ya Jambiani, Kusini Unguja.

Akizungumza katika makabidhianao hayo iliyofanyika shuleni hapo, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salam, Donatus Richard, alisema wameamua kutoa msaada huo ili kuunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuimarisha sekta ya elimu.

"Benki ya NMB tumeamua kushirikiana na jamii yote inayozunguka eneo la Jambiani kuchangia mabati 200 kwa ajili ya kutatua changamoto ya kuvuja kwa madarasa wakati wa mvua," alisema Donartus.

Aliongeza kuwa elimu ni kichocheo cha maendeleo, hivyo kuna kila sababu kwa watoto kupata mazingira mazuri ya kupata elimu na kusisitiza ndio maana benki ya NMB imeamua kuisaidia shule hiyo.

Nae Mwakilishi wa Jimbo la Paje ambae pia ni Waziri wa Kilimo, uvuvi, mifugo na umwagiliaji, Sudi Nahoda, aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo na kusema utasaidia kutatua changamoto ya kuvuja kwa shule hiyo.

"Nikuhakikishieni kuwa msaada huu mliotupatia una thamani kubwa na kiuhalisia NMB ni moja kati ya mashirika yanayojali jamii katika kuleta maendeleo," alisema Sudi

Kaimu mwalimu mkuu wa Shule ya Jambiani, Haji Haji, aliishukuru NMB kwa msaada huo, na kueleza kuwa kwa muda sasa wamekuwa wakikabiliwa na ubovu wa madarasa ambapo wanafunzi wamekuwa wakishindwa kuhudhuria masomo katika vipindi vya mvua.




Ukurasa 12

Jicho na mfumo ukusanyaji pesa za serikali usiopoteza hata 'senti'




**Lijue zao mpunga, namna lilivyo kinara wa uchumi**

Ukurasa 14

BUFE

IJUMAA FEBRUAR 19, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Waziri Mkuu awakumbatia Machinga na darasa la jicho, miwani ya Serikali kwao

## • Wanabeba robo nguvu kazi, pato taifa

**Na Sabato Kasika**

WAFANYABIASHARA wadogo, maarufu 'Machinga', wanatajwa kuwa muhimu na suluhisho la mahitaji kwa wengi, kuanzia wenye kipato cha chini, mpaka cha juu.

Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa nchi anasema sekta hiyo ina wajasiriamali milioni 3.1 na takwimu za viwanda na biashara zinaonyesha kuwa sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo zina mchango mkubwa katika ukuzaji uchumi na kuondoa umasikini nchini.

Kupitia kikao cha viongozi wa 'Machinga' nchini kilichoketi jijini Dar es Salaam, Majaliwa anasema wanaoajiriwa katika sekta hiyo ni asilimia 23.4 ya nguvukazi ya taifa na imechangia asilimia 27 katika pato la taifa, hivyo Serikali inatambua umuhimu wa wafanyabiashara wadogo katika maendeleo ya umma.

Kaulimbiu ya kikao ilikuwa 'Wamachinga ni fursa sahihi ya kujenga uchumi' wahusika wakiamini kwamba, utekelezaji wake utakuwa mwarobaini wa changamoto zinazowakabili.

Waziri Mkuu anawapa moyo kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi, ikiwamo vitambulisho vilivyokwishaanza. Anafafanua: "Napenda kuwahakikishia kwamba serikali inathamini sana mchango mkubwa wa sekta isiyo rasmi katika kuinua uchumi."

**MLANGO HALMASHAURI?**

Serikali inathamini mchango wa kada hiyo ya uchumi katika kuiongezea taifa mapato, huku baadhi ya halmashauri zinawakwamisha kwa kutowatengea maeneo ya kufanya biashara zao.

Ni mazingira yanayowafanya baadhi ya watu hao kuangukia kuvamia maeneo yasiyo rasmi, wakiendesha biashara, wenyewe waliomo kazini wanatetea msimamo kwamba kuna masoko mapya yanayokosa mahitaji kama vile maji, barabara na vyoo.



Wamachinga wakiendelea na shughuli zao. **PICHA: MTANDAO.**

Miaka kadhaa iliyopita, Waziri wa Ofisi ya Rais, mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Suleiman Jaffo, alizielekeza halmashauri zote nchini kuwatengea maeneo yenye miundombinu yote muhimu, kuondoa mivutano inayojitokeza kila mara baina ya halmashauri na wajasiriamali hao.

Hata hivyo, uhalisia hadi sasa ni kwamba 'Machinga' wameendelea kuzagaa mitaani katika maeneo yasiyo rasmi, sambamba na kusukumana na mamlaka za kiserikali.

Mfano mmojawapo ni wa wiki hii ambapo wamachinga wa eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam walivamia eneo la Barabara ya Bagamoyo, ambayo kwa sasa inapanuliwa na wamepanga bidhaaa zao, huku wakisukumana na wajenzi hao wa barabara.

**MIUNDOMBINU MUHIMU**

Kuna ukweli katika umuhimu wa kimarisha uchumi pasipo kuwapo na athari za kuchafua mazingira, ikiwamo kujisaidia ovyo na kutoa taka kienyeji, kutokana na ukosefu wa vyoo kwenye masoko pori wanakopatikana 'Machinga' wengi nchini.

Ni adha isiyozuilika kukuta umma wa watu wanaopatikana katika maeneo pori tajwa, wanajisaidia ovyo na kutupa chupa zenye uchafu na mengine mazito zaidi ya hayo.

Ni aina ya changamoto inayowabana 'Machinga' kuonyesha dhamira ya kuwainua katika utekekelezaji, ndipo inainuka nafasi na wajibu wa viongozi wenye dhamana, hasa katika halmashauri nchini kumaliza kero katika nafasi zao. Hao wanatakiwa kuhakikishe kwamba wanajenga masoko na kuweka miundombinu yote ili kusiwapo visingizio, ambavyo baadhi vinaangukia kuharibu mazingira ya umma.

Waziri Mkuu anawaambia Machinga kwamba, serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kushughulikia changamoto zinazowakabili, ikiwa ni pamoja na kuwawekea mazingira bora yatakayowawezesha kufanya biashara zao katika maeneo stahiki na mazingira sahihi.

Pia, anaitaka kada hiyo ya biashara kuwa na uzalendo kwa kutokubali kutumika katika sura ya kumsaidia mtu mwingine akwepe kulipa kodi, kwa kukubali kupokea bidhaa kutoka maduka makubwa pasipo kupatiwa risiti ya mauzo.

Majaliwa anawapa 'Machinga' elimu kwamba pale wanaporidhia kupokea bidhaa wanayonunua kutoka maduka hayo pasipo kudai risiti, ni kitendo kinachosaidia kukwepa ulipaji kodi, hivyo dawa sahihi ni kudai haki ya risiti yao.

Waziri Mkuu anasema, kada ya wafanyabiashara ndogo wamesaidia kutatua changamoto za ukosefu wa ajira kitaifa na kuwawezesha wapenda kazi wote akitaja mfano wa makundi ya vijana na kinamama, kuwa wanufaika.

Anasema ni kati yao, kuna wahitimu wa elimu ya ngazi za juu, kati na chini ambao wamekosa ajira nao kwa pamoja wanaingia katika safu ya kuajiriwa katika ujasiriamali huo, pasipo kubugudhiwa. Anataja dawa ya kuwa na vitambulisho maalum vinavyowahalalisha mkakati huo.

Waziri Mkuu anawataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini, wahakikishe wanapata takwimu sahihi za 'Machinga' waliopo katika maeneo yao, hali inayosaidia kuwarahisisha mpango mkakati na kazi ya utoaji vitambulisho vya biashara, wakiepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

UCHUMI

MAPINDUZI MAPYA YA GEPG;

# Jicho na mfumo ukusanyaji pesa za serikali usiopoteza hata 'senti'

- Mwenye akaunti 100, abakiza nane
- Mkusanyaji Sh.bil moja, sasa bil 2.5
- Mtumiaji aokoa gharama Sh.bil 38

GePG
Government electronic Payment Gateway

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

TAASISI kadhaa za serikali zimeeleza kufurahishwa na uanzishwaji na matumizi ya mfumo wa kielekroniki wa ukusanyaji mapato serikalini (GePG), kwamba umeleta tija, ufanisi na kuongeza makusanyo ya fedha za umma.

Inaelezwa, kuanzishwa mfumo huo ulioanza kutumika kuanzia mwaka 2017, umeleta mabadiliko makubwa katika ukusanyaji fedha za umma, ikiziba mianya ya 'mchwa' waliokuwa wanatafuna fedha za walipakodi,

Pia, inatajwa kuipunguzia gharama serikali kwa kuokoa muda wa wananchi katika kulipia huduma tajwa, kwani inaelezwa, Serikali ilikuwa inakutana na changamoto nyingi katika kukusanya mapato yake.

Katika hilo, kuna suala la watumishi waliopewa dhamana, baadhi waliokosa uadilifu hawakuwasilisha makusanyo halisi kutokana na mfumo wa kutumia risiti, ulikuwa rahisi kughushiwa.

Ilipoanzishwa matumizi ya mfumo huo, ni taasisi chache za serikali na halmashauri ndio zilianza kuutumia, lakini sasa zimeongezeka maradufu, kwa hesabu hadi mwaka huu, kuna jumla ya taasisi na halmashauri zaidi ya 682.




Mtaalamu wa Mfumo wa Malipo ya Serikali ujulikanao kama Government Electronic Payment Gateway (GePG App), Basil Baligumya, akitoa elimu kwa wahariri wa vyombo vya habari nchini, katika semina iliyofanyika jijini Arusha. Picha nyinginezo, ni kadi nja mfumo wakie wa malipo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**MREJESHO WAKE**

Kuna mrejesho unaojitokeza baadhi ya taasisi za umma zinaeleza kuufurahia mfumo huo kwa hoja umeleta ufanisi mkubwa katika kuongeza mapato yao mara dufu.

Hivi karibuni, wahariri kadhaa wa vyombo vya habari walihudhuria mafunzo ya mfumo huo jijini Arusha na walitembelea taasisi kadhaa kushuhudia matumizi yake na wakaelezwa jinsi ulivyowezesha kuongeza makusanyo.

Naibu Kamishna Msaidizi Huduma za Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Juma Kuji, anaipongeza serikali kuanzisha mfumo wa GePG, akisema umeongeza uwajibikaji na uwazi katika ukusanyaji mapato, ambayo yanaongezeka maradufu.

Kamisha Kuji anasema, kabla ya kuanza kutumika, mapato ya shirika lao, walikusanya kati ya Sh. bilioni 100 na 200 kwa mwaka, lakini baada ya kuanza kuutumia walifikia makusanyo wastani wa Sh. bilioni 364 kwa mwaka kabla ya ugonjwa wa Covid-19.

"Kabla ya mfumo huu wa GePG, tulikuwa na akaunti 100 za kukusanya makusanyo kupitia hifadhi zetu 22 na ilikuwa inatupa kazi kubwa ya kufanya mahesabu, pamoja kutumia gharama kubwa ya tozo za benki.

'Tulikuwa tunatumia muda mrefu kukusanya taarifa na kuandaa ripoti hata kuzipata fedha zenyewe... mara nyingi zilikuwa zinachelewa kuingia kwenye akaunti zetu," anasema Kuji (TANAPA).

Hivi sasa kamishna huyo ana mrejesho kuwa, mfumo huo umewanufaisha kwa kupunguza idadi kubwa ya akaunti za kuhifadhia benki, kutoka 100 hadi nane za sasa, nne ni za kukusanya fedha za ndani na nne makusanyo ya fedha za kigeni.

"Tuna mageti 22 nchi nzima na tulikuwa tunaendesha akaunti 100. Ilikuwa kazi kubwa kutengeneza taarifa zote, hizi ilikuwa lazima tutumie wahasibu kusimamia kila akaunti.

"Ila sasa gharama kubwa zimepungua na tunaweza kuona makusanyo yetu sasa kwa muda mchache na kwa uwazi na hakuna gharama tunazotoa na ripoti zinapatikana mara moja," anasema.

Kamishna Msaidizi Mwanadamizi Mkaguzi wa ndani, Christopher Mtibili, anasema mfumo huo wa GePG umewezesha kuongeza mapato kupitia makusanyo na kuchangia pato la taifa.

Anasema, kabla ya mfumo wa sasa walikuwa wakipata changamoto akaunti za malipo zilikuwa nyingi, tofauti na sasa ambapo wanatumia anachokiita 'Control number' (namba ya kusimamia).

**MKUU TEHAMA**

Kwa upande wake ofisa Mwanadamizi Uhifadhi (TEHAMA), Boniface Mariki, anasema mfumo GePG umewawezesha waongozaji watalii kuokoa muda na kulipa kabla ya kupata huduma na kwamba hata yanapokuwapo makossa ya kiufundi ni rahisi kurekebisha kupitia mfumo huo.

"Wafanyabiashara wengine walikuwa wanataka huduma kwanza, kisha kulipa baadaye, lakini kutokana na mfumo huu huwezi kupata huduma yoyote bila kulipia... utalipa kwanza ndio upate huduma, maana hakuna mazungumzo, hivyo hasara hakuna kabisa," anaeleza.

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA), Ndaki Tito, anasema tangu wajiunge GePG, wameongeza makusanyo kutoka Sh. bilioni 1.2 hadi Sh.bilioni 1.6 kwa mwezi.

"Mbali na kutoongezea mapato, mfumo umetusaidia sana kupunguza rasilimali watu, ambao walikuwa na kazi ya kuhudumia wateja, kwa sasa wamepangiwa kazi nyingine," anasema.

Ndaki anafafanua kuwa ni mfumo uliompunguzia muda wa mteja badala ya kufika ofisini kulipia gharama za maji, inatumika njia ya mitandao mbalimbali waliyo nayo na matumizi ya risiti za karatasi.

**MDAU MTUMIAJI**

Msajili wa Wanafunzi katika Chuo cha Ufundi Arusha (ATC), Dk. Baraka Kichonge, anasema tangu waanze kutumia mfumo huo, wameongeza ukusanyaji mapato na kuboresha utendaji kazi wao.

Mhasibu wa Chuo hicho, Said Ngonyani, anasema GePG imewaweka mbali wazazi na udanganyifu kutoka kwa baadhi ya watoto wao ambao ni wanafunzi kwenye ulipaji wa ada.

"Sasa hakuna tena tatizo hili, maana chuo kinatoa 'control number' na wanapolipa wanapata risiti za elektroniki," anasema Ngonyani.

Kwa mujibu wa Ngonyani, ni mfumo mkombozi kwa wazazi dhidi ya uongo wanawadanganya, hoja kupotea fedha walizopewa kwa njia tofauti

**KATIBU MKUU FEDHA**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, anasema matumizi ya mfumo huo kwa taasisi na halmashauri nchini, umewezesha ongezeko la mapato, hatua iliyowezesha kufanikishwa utekelezaji miradi mikubwa ya kimkakati kitaifa.

"Mfumo wa ukusanyaji wa fedha unapoboreshwa, unawezesha nchi kukusanya kiasi kikubwa cha mapato ya ndani na kwa ufanisi mkubwa na kurahisisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo," anasema Katibu Mkuu.

Anarejea kuanzishwa mfumo huo, ilikuwa kuboresha ukusanyaji mapato kirahisi na kuondokana na gharama kubwa za miamala ya fedha za umma, mlolongo wa utaratibu usio rafiki kwa mlipaji huduma za umma, namna ya kutoa ankara, jinsi anavyolipia ankara na anavyopatiwa stakabadhi yake.

Doto anasema mfumo wa awali haukutoa taarifa sahihi na kwa wakati wa makusanyo na kwa uwazi unaotakiwa, tofauti na sasa, GePG imeunganishwa na taasisi za maeneo mbalimbali, ikiwamo serikali za mitaa na taasisi nyinginezo serikali kuu.

Katibu Mkuu anashauri, ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za serikali, Watanzania waanze kutumia mfumo huo mpya serikalini kulipia huduma na kuepuka fedha za rushwa na malipo kutofika serikalini.

Doto anatoa mfano wa taasisi iliyonufaika na uanzishwaji mfumo huo kuwa ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kwa mwaka mmoja imeokoa Sh. bilioni 38 walizokuwa wakiwalipa wakala, wakiwamo wa vipimo nchini, huku makusanyo yako juu zaidi, kutoka Sh. bilioni moja ya zamani, hadi Sh.bilioni 2.5 za sasa.

Mkurugenzi wa Mifumo ya Fedha na Mipango kutoka Wizara hiyo, John Sausi, anasema wakati umefika kwa Watanzania kutumia mfumo huo, ili kuwa na uhakika wa malipo yao.

Anataja mafanikio kadhaa waliopata tangu kuanzishwa mfumo huo ni kuokoa fedha nyingi za serikali, zimekuwa zikipotea kabla ya mfumo huo na kuiwezesha serikali kupata na kuona taarifa zinazohusu ukusanyanji wa mapato nchini kwa wakati.



TAFAKURI YA MLALAHOI

## Magereza msichezee fursa ya Magufuli






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

AKIZINDUA majengo ya Jeshi la Magereza mkoani Dodoma, hivi karibuni, Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais John Magufuli, alieleza kufurahishwa na kinachoendelea kufanywa na jeshi hilo, hususan katika uanzishwaji na ukamilishaji miradi ya maendeleo.

Alizindua ujenzi wa nyumba za askari Magereza Isanga, kiwanda cha samani Msalato na makao makuu ya Magereza, ambako kote alishuhudia jinsi miradi hiyo ilivyokamilika tena kwa kiwango kidogo cha fedha. Bila kuficha hisia zake, akasema, kwa mara ya kwanza jeshi hilo lilimfurahisha.

Pia, alisikiliza kero mbalimbali zinazolikabili jeshi hilo, ikiwa ni pamoja na madeni yanayozidi taasisi mbalimbali za serikali. Rais aliamua kubeba mzigo huo na kuzitaka zilipe madeni, la sivyo atazikata mwenyewe na kulilipa jeshi hilo.

Kero nyinginezo ziligusa askari mmoja mmoja, ikiwa ni pamoja na nyumba mbovu, sare na hata chakula, ambapo alishangaa kwani kero hizo ziko chini ya uwezo wa jeshi na kinachotakiwa ni ubunifu na kujipanga, akisisitiza matumizi mazuri ya nguvu kazi iliyopo.

Alitoa mfano wa kujitosheleza kwa chakula kwa kutumia wafungwa, lakini hata kujishonea sare kwa kuwatumia hao hao, akisisitiza kuwa wengi wao hufungwa wakiwa na taaluma zao zinazoweza kutumiwa kwa manufaa ya jeshi, kwa maana yawafungwa na askari Magereza.

Alishangaa iweje mke wa askari aonekane barabarani akienda sokoni kununua chakula, huku wafungwa wanaweza kukizalisha wakala na kusaza na kingine kuliwa na askari.

Hali kadhalika wafungwa mafundi cherehani kukaa bila kushona, huku magereza wakiwa na uwezo wa kununua vyerehani na kuvitumia.

Naunga mkono kwa asilimia 100 kauli ya Rais Magufuli ya wafungwa kutumiwa katika uzalishaji wa kila kitu, wakati wote wakitumikia vifungo vyao magerezani, kwani hawahitaji gharama yoyote kutokana na ukweli kuwa, hawalipwi mishahara wala posho, zaidi ya kula na kulala bure.

Endapo wafungwa watazalisha chakula wakajilisha na kupata nguvu, ndivyo watakavyofanya kazi na kuzalisha bidhaa, zingine zikatumiwa hata katika taasisi za serikali hususan samani na kuacha kutumia fedha za kigeni kuziagiza nje.

Wanapokuwa magerezani, taaluma walizo nazo watazienddeleza na kupata ujuzi zaidi na mara wamalizapo vifungo, kwa kawaida au kwa msamaha, wanaporudi majumbani waanzishe miradi ya kujikimu kimaisha na kusaidia jamaa na ndugu zao na Taifa kwa jumla.

Yawezekana ile dhana kwamba magerezani ni mahali pa kutoa adhabu, bado imejikita ndani ya akili za baadhi ya Watanzania wanaopaona si pa kuwarekebisha tabia na kuwa watu wema mara watokapo.

Ifahamike, kama alivyobainisha Rais Magufuli, magerezani ni mahali ambako mtu yeyote anaweza kwenda bila ya kujali taaluma aliyo nayo, lakini ni fursa kwa taaluma hizo kutumiwa vizuri kulisaidia Taifa na mtu mmoja mmoja.

Kama wafungwa watatumika vema, ni wazi wafanyakazi wa magereza wataishi maisha mazuri, kwani watapata kila kitu kuanzia chakula mpaka samani kama si bure, lakini kwa bei nafuu na mishahara yao ikatumika kusomesha watoto na mambo mengine. Kupanga ni kuchagua. Hili linawezekana. Alamsiki!

BIASHARA

# Lijue zao mpunga, namna lilivyo kinara wa uchumi

## • Simulizi ya Kahama na soko nchi jirani

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MPUNGA umo kati ya mazao makuu ya kimkakati nafasi nzuri katika uchangiaji Pato la Taifa na matumizi ya moja kwa moja.

Pia, ni zao la pili kulisha umma, ikifuatiwa na mahindi na inaelezwa inatumika kulisha kaya nyingi kitaifa. Wazalishaji ni wakulima wadogo wanaotegemea soko la wasindikaji wanaohifadhi bidhaa ghalani.

Wilaya ya Kahama, imo katika wanakolima na kuna viwanda vya uchakataji na kusindika, ikilisha mikoa na nchi jirani za maziwa makuu, kama vile Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Uganda.

Madalali na wafanyabiashara wa zao hilo, nao wamekuwa wakienda moja kwa moja shambani.

Baraza la Mchele Tanzania (RCT) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti REPOA, kupitia mradi unaoitwa, TradeCom II unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), waliandaa mafunzo ya wasindikaji 100 nchini kuwajengea uwezo wazalishe mchele wenye viwango bora, kukidhi ushindani sokoni, ndani na nje ya nchi.



Wasindikaji mchele kutoka Kanda ya Ziwa, wakiendelea na mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuzalisha mchele bora wenye viwango vinavyokidhi ushindani, yanayoendeshwa na Baraza la Mchele Tanzania na Taasisi ya REPOA.

### BARAZA LA MCHELE

Winnie Bashagi ni Mkurugenzi wa RCT, anasema zao hilo linachangia pato la taifa kwa asilimia 2.6 na walimaji ni wakulima wadogo wa wilaya 64 na zaidi ya kaya asilimia 18 wanufaika nayo.

Anasema, uzalishaji mkubwa wa mchele uliingia nchini mwaka 1884, ikitumika kama zao la chakula na hadi sasa inalimwa kwa wingi kulinganisha na mahindi kwa wakati huo.

Bashagi anasema, uzalishaji wake unafuatiwa na mahindi na kila mwaka uzalishaji huo umekuwa ukiongezeka, hata kufafanua uwapo wa ziada ya chakula hicho.

Anasema mwaka 2007, serikali iliacha kuagiza mchele kutoka nje ya nchi, baada ya uzalishaji kuongezeka maradufu hata wakaacha kutegemea msimu wa mvua pekee wa kuegemea kilimo.

Vilevile anasema kila mkulima anapolima zao hilo kupitia mbinu ya umwagiliaji, zao linapatikana wastani wa mara mbili ya ilivyozoeleka katika utegemezi wa msimu.

Bashagi anasema, katika msimu uliopita walipata ongezeko la tani milioni 1.2 za mpunga na kusababisha kuwa na ziada ya zao hilo na msimu uliopo walipata ziada ya tani milioni 1.8 na hapo ni baada ya eneo la Kilombero kutopata mavuno mazuri.

"Nchi hii ina zaidi ya hekta milioni 21 za kulima zao la mpunga lakini zimetumika hekta milioni 2.1 na kusalia kuwa na eneo kubwa sana.

"Sisi tutaendelea kuwahamasisha wakulima kulima zaidi ili kuwa na mchele wa kutosha ambao utapelekwa kwenye ushindani wa masoko ya kimataifa," anasema Bashagi

Pia, anaongeza kwamba:"Wanaendelea kutoa mafunzo kwa wasindikaji mchele, ili kuwajengea uwezo waweze kuzalisha mchele bora wenye viwango vinavyokidhi ushindani wa masoko ya ndani na nje. Kati ya wilaya 64 zinazolimwa mchele, wilaya 13 ndizo zinazopewa mafunzo haya.'

### TAASISI REPOA

Stephen Mwombela, ni Mtafiti kutoka taasisi ya REPOA nchini, anasema kabla ya kutolewa mafunzo kwa wasindikaji mpunga Kanda ya Ziwa, walitafiti zao na wakagundua wasindikaji wengi hawana elimu ya kisasa inayohitajika kwenye soko la ndani na nje.

Anasema, mafunzo yanalenga kuwajengea uwezo watunga sera, wazalishaji na wauzaji bidhaa za ndani na kuboresha na kupanua masoko na ushindani wake kitaifa na kimataifa, ukitanua mnyororo wa thamani kwenye mazao ya mboga, ngozi, usafirishaji Zanzibar.

Mwombela anasema, kwa kushirikiana na Baraza la Mchele Tanzania (RCT) walitafiti mahitaji ya mchele na kubaini uhaba wa masoko ya uhakika ndani na nje, kisa kikuu ni kukosekana elimu ya usindikaji.

"Wasindikaji tulio nao hawatambui namna bora ya usindikaji, kulingana na viwango vya kimataifa vinavyohitajika kwenye masoko ya kimataifa.

"Ndio sababu tunatoa elimu ya usindikaji wa kutumia mashine za kisasa, leo tuko na wasindikaji kanda ya ziwa na baadae tukakuwa na wakulima wa Morogoro, Iringa na Mbeya," anasema.

### WASINDIKAJI KANDA

Mfanyabiashara na msindikaji kutoka Shinyanga, Victor Muzo, anaiomba serikali kuunda ushirika kwa wafanyabiashara au wasindikaji mchele, ili kuwa na bei ya pamoja itakayosaidia masoko ya uhakika kutoka nchini za Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara (SADC)

Anasema kila mmiliki wa mashine ya kusindika mchele hivi sasa ana bei yake ya kuuza mchele, hali inayowafanya wateja wasiwe na bei moja.

"Maisha yetu yameshikiliwa na madalali wanaotupangia bei hasa tunapopata tenda kubwa na tunashindwa kukataa, kwa sababu kila mashine inayosindika mchele ina bei yake. Tunaomba serikali kutengeneza ushirika ili tuwe na bei moja na yenye tija," anasema Muzo.

Haroun Msuya, ana maoni kwamba mchele umekuwa ukishuka bei kutokana na uhaba wa soko ya uhakika ya ndani na nje, inayoleta hitilafu katika uvukaji mpaka na ugumu wa kufikia ng'ambo, ikihusisha nchi za Rwanda, Kenya, Uganda na DRC.

Pia, Asha Hassani anasema eneo walikojenga viwanda vya uchakataji mchele, ni katikati ya mji na halikidhi mahitaji. Hivyo, anaiomba serikali kuwatengea eneo lingine wajenge viwanda vikubwa na kuwatafutia mikopo yenye riba nafuu wawekeze.

### CHANGAMOTO NI ZIPI?

Haroun Msuya, anasema kukatika umeme wakati wa kokoboa au kusindika mchele kimechangia hasara kubwa baada ya kusimama kwa muda mrefu hasa pale wanapopata tenda kutoka kwa wafanyabiashara wakubwa wahitaji.

Vile vile anasema kuwa, wanakosa masoko ya uhakika baada ya Serikali kuwazuia wanunuzi wa mchele kutoka nje na kuweka tozo kubwa ambazo zinasababisha kushindwa kusafirisha mchele kimataifa na kubaki na mpunga mwingi kwenye maghala.

Victor Muzo anasema serikali inatakiwa kuweka wazi tenda za usambazaji chakula katika shule za serikali na binafsi, ikiwa njia mojawapo kutanua soko la zao hilo.

Pia mdau Asha Hassani, anasema changamoto nyingine ni wafanyabiashara kutoka nchi jirani, wana tabia ya kwenda moja kwa moja kwa mkulima shambani na kumrubuni na kununua mpunga kwa bei wanayoitaka.

### KATIBU TAWALA

Aliyefungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama Timothy Ndanya, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa Shinyanga, anasema serikali imekuwa ikitengeneza mazingira bora kwa wakulima, ili waongeze uzalishaji na kipato kwenye kaya.

Ndanya anasema, changamoto za kukatika umeme na kusababisha kusimama shughuli za uzalishaji wakati wa uchakataji mchele na atahakikisha anazifikisha kwa Meneja wa Tanesco Kahama, aangalie namna ya kukabiliana na tatizo hilo.

Anawataka kuwa na uhusiano bora na wakulima wa zao hilo katika sehemu zote zinazolima mpunga na kuacha kulima kwa kutegemea mvua

Katibu Tawala huyo, anawashauri wazalishaji mpunga hao, watumie vyema kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi kilichopo kata ya Nyihogo, Halmashauri ya Mji wa Kahama, ili kuongeza thamani ya mchele wao sokoni.




Mkurugenzi wa Baraza la Mchele Tanzania (RCT), Winnie Bashagi, akiendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kuzalisha mchele bora unaokidhi soko la ndani na nje kwa wasindikaji wa mchele wilayani Kahama. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**



# Serikali yataka asasi za kilimo kubainishwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amewaagiza watendaji wa Wizara hiyo kuhakikisha kila shirika lisilo la kiserikali linaloweka fedha kwa ajili ya kilimo zibainishwe ili kuepusha mkanganyiko wa utekelezaji wa miradi.

Bashe alitoa maelekezo hayo jana alipokutana na wadau wa zao la chai baada ya Serikali kupokea msaada wa kutoka Umoja wa Ulaya (EU) wa Euro milioni 100 kwa ajili ya kuboresha sekta ya kilimo kwenye zao la chai ambapo mradi utatekelezwa kwa miaka minne.

Alisema lazima kila fedha inayoingia ijulikane ili ilete matokeo yanayotarajiwa.

"Mradi huu kwa kuwa ni wa miaka minne maana yake kila mwaka zitatumika Euro milioni 25, tumewaita hawa wadau kuona hizi fedha zinaelekezwa maeneo gani na sehemu kubwa ya hizi fedha Euro milioni 48 zinakwenda kwenye ujenzi wa barabara," alisema.

Alisema suala la barabara ni muhimu sana kwenye zao hilo kwasababu kilo milioni nne ya chai kwa mwaka imekuwa ikitupwa kwa kukosekana miundombinu ya barabara ya kusafirisha zao hilo.

Hata hivyo, Naibu Waziri alisema kikao hicho serikali imeshauri wadau kupunguza gharama za uendeshaji ikiwamo semina ili fedha hizo zielekezwe kwenye miundombinu.

Bashe alisema wataendelea kujadiliana na wadau hao mambo mbalimbali ili kuwe na tija kwa wakulima wa zao hilo.

Alisema mradi huo utaingiza miche milioni 1.5 ya chai kwa wakulima na Bodi lazima ihakikishe matokeo yanaonekana.

Alisema Umoja huo umeeleza utayari wa kuanzishwa kwa soko la chai Tanzania na litaanza mwaka huu.

"Tunataka tujue kila shirika lisilo la kiserikali na kila mfadhili anayeweka fedha anaiweka wapi na matarajio yake ni yapi kuliko kuwapo na mwingiliano wa mradi kufanyika na mashirika mengi, haina mantiki," alisema.

Aidha, alisema timu ya Wizara inafanya kazi ili kuonesha maeneo muhimu ya kipaumbele na wafadhili wote watafuata maelekezo hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma, Jabiri Shekimweri, akizungumza na wanafunzi, walimu na wazazi wa Kijiji cha Mkutupa, wilayani humo jana, baada ya kupokea msaada wa madawati kutoka benki ya NMB. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Katazo la michango shuleni lasisitizwa

**Na Ibrahim Joseph,** MPWAPWA

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabiri Shekimweri, amepiga marufuku wakuu wa shule na kamati kuchangisha michango kwa wazazi bila kibali maalum.

Pia, amepiga marufuku mwanafunzi kufukuzwa shule kwa kigezo cha kutolipa michango kwa sababu inaleta malalamiko kwenye jamii.

Shekimweri alisema hayo juzi wakati akipokea msaada wa vifaa mbalimbali vilivyotolewa na Benki ya NMB wilayani hapo.

Mkuu huyo wa Wilaya alipiga marufuku wakuu wa shule na Kamati za shule kuchangisha michango kwa wazazi kwa kuwa inasababisha malalamiko kwenye jamaii.

"Ni marufuku kuchangisha michango wazazi au kumfukuza mtoto kwa kigezo cha kushindwa kulipa michango ya shule, kama kuna tatizo lolote kamati za shule zinatakiwa kuomba kibali cha kuchangisha michango," alisema.

Alisema anajua shule nyingi zinakabiliwa na upungufu wa mahitaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na madawati ,viti na meza kwa wale wa sekondari lakini wazazi na kamati husika za shule wanatakiwa kukaa pamoja na kuomba kibali cha kuchangisha.

"Sasa hivi kuna tatizo la wanafunzi wanaoingia kidato cha kwanza kuchangishwa viti na meza, hii sio sawa, kuna wengine wanashindwa kufika kuanza masomo kwa kigezo cha kukosa michango hiyo"alisema

Aidha, aliwataka maofisa elimu kata kuhakikisha wanatembelea maeneo ya shule wanazozisimamia ili kubaini matatizo yaliyopo.

Aliwataka kukagua madawati, viti na meza vilivyojaa kwenye stoo kwa madai kuwa vimeharibika wakati matengenezo yake yapo chini ya uwezo wa shule husika.

"Ukitembelea shule zetu hizi utasikia tunaupungufu wa madawati wakati ukitembelea stoo kuna viti na meza pamoja na madawati mengi yanahitaji ukarabati kidogo na shule husika wanaweza kuifanya," alisema.

Kadhalika, aliwataka maofisa elimu kata kufanya kazi ya kusimamia nidhamu mahali pa kazi ili kuhakikisha wanapandisha kiwango cha ufaulu wa wanafunzi.

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Paul Sweya, alisema wana upungufu wa madawati zaidi ya 2,000 na sekondari wana upungufu viti na meza zaidi ya 3,000.

Hata hivyo, Sweya alisema walifanya mkutano na baadhi ya wadau wa maendeleo pamoja na wafanyabiashara wilayani hapo na kuahidi kuwa upungufu wa meza, viti na madawati utatatuliwa. Aliongeza wanafunzi wote waliokuwa wamechaguliwa na kukosa nafasi ya kujiunga, kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa wataingia wote shule mwezi huu.

## Vijana watakiwa kuchangamkia fursa ya mikopo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIJANA wametakiwa kutumia fursa ya mikopo inayotolewa na Halmashauri nchini ili kujikwamua kiuchumi badala ya kukaa vijiweni na kujiingiza kwenye uhalifu.

Akizungumza katika warsha ya vijana ilioandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Endlless Success Foundation, Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Amina Feruz, alisema halmashauri zinatoa fedha hizo ili kuwasaidia vijana kupanua wigo wa kuendeleza shughuli za ujasiriamali badala ya kutegemea ajira pekee.

Aliwataka vijana kuunda vikundi kuchangamkia fursa hiyo ambayo itawasaidia kuwapa mwongozo wa kubadili fikra potofu ya kusubiri kuajiriwa.

"Vijana tumieni fursa ya mikopo inayotolewa na serikali kupitia halmashauri kubuni miradi ya kufanya,hii itawasaidia kujikwamua kiuchumi badala ya kusubiri ajira,"alisema Feruz.

"Awali sheria ya utoaji mikopo ya asilimia 10 katika halmashauri wakopaji walilazimika kuwa na biashara, lakini hivi sasa sheria hiyo inaelekeza mtu kuwa na andiko la mradi anaotaka kufanya kupitia mkopo anaotarajia kukopa, na kuwapo kwenye kikundi," alisema.

Alisema wao kama Taasisi wapo kwa ajili ya kuwapa muongozo vikundi vya vijana ya namna ya kupata mikopo hiyo ikiwamo kuwakutanisha na wataalamu kulingana na mradi wanaohitaji kufanya.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi yao pia hufanya kazi ya kutoa elimu ya usimamizi wa fedha kwa vikundi vya vijana ambao wako katika taratibu za uchukuaji mikopo ya kufanyia biashara zao za kila siku.

Kwa upande wake, mmoja wa washiriki wa warsha hiyo, Juma Mrisho, aliishukuru halmashauri kwa kubadili sheria ya utoaji mikopo kwa vijana ambayo itachangia vijana kubuni miradi ya biashara yenye matokeo chanya.

Mrisho alisema vijana wengi wana uwezo wa kufanya biashara katika maeneo wanayotoka, lakini tatizo kubwa linayowakabili ni ukosefu wa mitaji, ambapo hivi sasa serikali imewarahisishia badala kuwa na biashara wanawasilisha wazo lenye michanganuo.





## Barabara yawatia matumaini Mbalizi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wanaotumia barabara ya Mbalizi- Mkwajuni, wameanza kupata matumaini ya kuondokana na adha ya kukwama mara kwa mara njiani baada ya Serikali kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe. Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya watumiaji wa barabara hiyo walisema magari yamekuwa yakikwama kutokana na barabara hiyo kuwa mbovu kwenye baadhi ya maeneo na hivyo kusababisha wachelewe kufika safari zao.

Mmoja wa wananchi hao, Jordan Msako, alisema mara nyingi mvua ikinyesha mito huwa inajaa na kupita juu ya madaraja hali ambayo husababisha mawasiliano kukatika mara kwa mara. Alisema kwa sasa wameanza kupata matumaini ya barabara hiyo kuboreshwa baada ya Wakala wa Barabara, (TANROADS) kuweka mabango yanayoashiria kuanza kujengwa kwa barabara hiyo ambayo inaunganisha mikoa ya Mbeya na Songwe.

"Kuna vibao vimewekwa ambavyo vinaonyesha kuwa barabara hii itajengwa kwa awamu mbili ambazo ya kwanza itaanzia katika Mji wa Mbalizi mpaka Chang'ombe na awamu ya pili itaanzia Chang'ombe mpaka Makongolosi wilayani Chunya," alisema Msako.

Naye Helen Sabath, mfanyabiashara katika Mji wa Mkwajuni wilayani Songwe, alisema kipindi cha mvua hata gharama za usafiri zimekuwa zikiongezeka kutokana na barabara hiyo kuwa mbovu.

Alisema wao wanategemea kununua bidhaa wanazoziuza katika Mji wa Mbalizi lakini wakati wa usafirishaji huwa ni tatizo hivyo aliishukuru Serikali kwa kuamua kuanza kuijenga barabara hiyo japo kwa kiwango cha changarawe.

Alisema wakati mwingine mawasiliano ya barabara hiyo yamekuwa yakikatika na hivyo kuwalazimu kuzungukia wilayani Chunya ambako kunakuwa mbali na kusababisha gharama za usafiri kuongezeka.

"Tunaamini kwamba baada ya barabara hii kukamilika tutakuwa tunatumia muda mfupi sana kufika Mbalizi na kurudi nyumbani, magari sasa hivi yako mengi lakini taizo ni barabara tu," alisema Helen.

Mara nyingi Mbunge wa Jimbo la Songwe, Philip Mlugo na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, wamekuwa wakiomba Serikali kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili kuwapunguzia wananchi matatizo ya usafiri.

# Vyanzo vya maji vyalindwa na kamera

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-UWSA), imeanza kutumia kamera za usalama kulinda baadhi ya vyanzo vya maji ili kuzuia uharibifu wa mazingira kwenye vyanzo hivyo pamoja na wizi wa vifaa na mitambo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Ndele Mengo, aliyasema hayo juzi wakati wa ziara ya wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi wa mamlaka hiyo kwenye vyanzo vya maji vya Nzovwe na Mwashali jijini humo.

Alisema katika Jiji hilo kuna vyanzo vya maji 15, lakini mpaka sasa vyanzo 14 vimeshafungwa kamera hizo na kimoja kilichobaki wanaendelea na mipango ya kufunga ili kuhakikisha vyanzo vyote vinakuwa salama.

Mhandisi Mengo alisema kuna mtaalamu wa mamlaka hiyo ambaye anafanya kazi ya kufuatilia kila kinachorekodiwa na kamera hizo kwenye maeneo husika ili kuhakikisha hatua zinachukuliwa mapema kudhibiti uharifu.

"Tumefunga kamera za usalama kwenye vyanzo vyetu, sasa hivi kuna mtu ambaye anafuatilia matukio yote na hata sasa tupo hapa anatuona kila tunachokifanya, kwahiyo vyanzo vyetu vyote viko salama, mbali na hizo kamera pia tuna kampuni ya ulinzi ambayo inalinda vyanzo vyetu," alisema Mhandisi Mengo.

Aidha Mhandisi Mengo alisema Mamlaka hiyo inaendelea na utekelezaji wa miradi miwili ya Nzovwe na Mwashali-Isyesye ili kumaliza tatizo la maji kwenye maeneo ya miinuko zikiwemo Kata za Isyesye, Gombe, Ilemi na Itezi.

Alisema mradi wa Nzovwe unatarajiwa kukamilika Februari 28 na wa Mwashali- Isyesye unatarajiwa kukamilika Machi 15, na kwamba miradi hiyo ikikamilika itaongeza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa wananchi katika Jiji hilo pamoja na Mji wa Mbalizi kutoka asilimia 80 za sasa mpaka asilimia 87.

Alisema maeneo yanayolengwa kunufaika na miradi hiyo miwili yamekuwa yakipata maji siku mbili pekee kwa wiki na kwamba baada ya miradi hiyo kukamilika wananchi watakuwa wanapata maji saa 24 siku zote saba za wiki.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mbeya-UWSA, Edina Mwaigomole, aliipongeza menejimenti ya mamlaka hiyo kwa utekelezaji na usimamizi wa miradi kwa kutumia wataalamu wa ndani kwa maelezo kuwa utaratibu huo unasaidia kuokoa fedha nyingi.

Alisema Mamlaka hiyo ni miongoni mwa mamlaka chache nchini ambazo zinajitegemea kwa asilimia 100 hivyo akawataka watendaji kuendelea kushirikiana ili wananchi waendelee kupata huduma bora na walipie huduma kwa haki.

Aliwataka wananchi kuendelea kulipia huduma hiyo ili kuifanya mamlaka hiyo iendelee kuwahudumia kwa viwango vinavyostahili na kutekeleza miradi mingine ambayo itasaidia upatikanaji wa maji kufikia asilimia 100.

"Sisi kama Bodi tumeridhika na utekelezaji wa miradi yote tuliyotembelea, tumejaribu kulinganisha vitu mlivyotuandikia kwenye makabrasha na uhalisia wa miradi yenyewe tumeona vinawiana vizuri, ushirikianao huu uendelee ili wananchi waifurahie mamlaka," alisema Mwaigomole.

Kwa upande wake, Hilda Ngowi, ni Mjumbe wa Mamlaka hiyo, alishauri menejimenti ya Mamlaka hiyo kuendelee kutunza mazingira kwa kupanda miti kwenye vyanzo vyote vya maji ili miradi inayotekelezwa iwe endelevu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-UWSA), Ndele Mengo (wa tatu kulia), akiwaonyesha wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi wa mamlaka hiyo, moja ya mitaro ambayo inaendelea kuchimbwa kwa ajili ya mabomba yatakayokuwa yanapeleka maji kwenye Kata za Isyesye, Itezi, Ilemi na Gombe. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC: Wafanyabiashara msiiogope TRA

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imewashauri wafanyabiashara kutowaogopa maofisa wa Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) na badala yake wawape ushirikiano kwa kutoa nyaraka zinazohitajika ikiwamo risiti za mauzo ili wakadiriwe kodi kwa usahihi.

Aidha wafanyabiashara hao wameshauriwa kuwaeleza maofisa wa TRA matatizo yanayowakabili kwenye biashara zao hasa kuhusu masuala ya kodi ili yapatiwe ufumbuzi ili kukuza biashara zao na kulipa kodi itakayosaidia kutekeleza miradi ya maendeleo.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati maofisa wa TRA kutoka Mkao Makuu na wa Mkoa wa Mbeya walipokuwa wanatoa elimu kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa na tabia ya kufunga maduka yao na kutimua mbio pale wanapowaona maofisa wa TRA hali ambayo ailidai inafifisha ufanisi wa mamlaka hiyo kwenye utekelezaji wa majukumu.

Alisema maofisa wa TRA hawawezi kutembea madukani kukusanya kodi kwa wanunuzi wa bidhaa madukani na badala yake inawafanya wafanyabiashara kuwa mawakala wa kukusanya kodi kwa kutoa risiti kila wanapouza bidhaa zao.

"Serikal imekuamini wewe mwenye duka ukusanye kodi kwa wanaonunua bidhaa kwako kisha uiwasilishe TRA kwa pamoja, sasa unapowakimbia maofisa hao wanapokuja kukutembelea unakuwa umeharibu sana," alisema Chalamila.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Eunice Liheluka, alisema wapo baadhi ya wafanyabiashara mkoani humo ambao ni wajeuri kwa kukwepa kutumia mashine za kielektroniki za ukusanyaji wa mapato na hivyo kusababisha upotevu wa mapato.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuacha kukwepa kutoa risiti hizo kwa maelezo kuwa watakumbana na adhabu kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kutozwa faini na kufungiwa biashara kwa mujibu wa sheria za kodi.

"Sisi huwa hatupendi kutoa adhabu lakini wafanyabiashara mnatulazimisha kutoa adhabu hizo ambazo wakati mwingine zinakwamisha biashara zenu, nawashauri mjitahidi kufuata sheria za nchi," alisema Liheluka.

Ofisa Elimu kwa mlipakodi kutoka TRA Makao Makuu, Jamsi Ntalika, alisema wanafanya mikutano na wafanyabiashara nchi nzima ili kubaini matatizo yanayowakabili ikiwamo matatizo ya kodi na yasiyokuwa ya kodi.

Alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuboresha biashara za wananchi ili zikuwe na wawe na uwezo wa kukuza biashara na kulipa kodi serikalini na kuendesha maisha yao.

Alisema watahakikisha wanawatembelea wafanyabiashara katika mikoa na wilaya zote nchini ili wayatambuwe matatizo yanayowakabili wafanyabiashara na kuyatatua haraka.

Baadhi ya wafanyabiashara waliohudhuria mkutano huo, baadhi ya wafanyabiashara waliiomba Serikali iwapunguzie kodi hasa ya ongezeko la Thamani (VAT) wakidai kuwa inawakwamisha kwenye shughuli zao.





Wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, wakiwa wamejipanga barabarani nje ya ofisi hiyo, Migombani jana, wakisubiri mwili wa Maalim Seif Sharif Hamad aliyefariki juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yatilia shaka kampuni ya usafi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Mkoa wa Mjini Magharibi, umeeleza wasiwasi wake juu ya uwezo wa kampuni ya Green Weste Pro Ltd kuhusu kufanya usafi katika manispaa ya Wilaya ya Mjini iliyopewa mkataba wa kufanya kazi hiyo.

Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, alieleza hayo juzi kufuatia ziara aliyoifanya katika maeneo mbalimbali ya nyumba za maendeleo Michenzani na Kilimani na kushuhudia kuwapo kwa mrundikano na kuzagaa kwa taka katika maeneo hayo.

Alisema haiwezekani mji kuwa katika hali ya uchafu wakati serikali imeingia mkataba na kuilipa fedha kampuni hiyo ya usafi, lakini uwezo na vifaa vya kusafisha ni kidogo na kupelekea kurudisha nyuma juhudi za serikali katika kuweka usafi wa mji.

"Serikali kupitia Manispaa ya Mjini imeamua kubinafsisha suala la taka ili kuweka mji wetu katika mazingira mazuri kwa vile manispaa yenyewe ilionekana kushindwa kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi, lakini kampuni yenyewe nayo inaonekana kuwa na uwezo mdogo wa kufanya usafi na vifaa haina," alisema mkuu wa Mkoa.

Aidha mkuu wa Mkoa huyo ametoa wiki mbili kwa uongozi wa kampuni ya Green Weste Pro kuhakikisha wanajipanga vizuri kuona wanafanya kazi hiyo kwa ufanisi na ikishindwa Serikali inafuta mkataba wao.

"Natoa wiki mbili mjipange vizuri nione kazi hii inafanyika kama serikali inavyotarajia kuona mji huu unakuwa safi, lakini pia majaa yote tuliotembelea leo muhakikishe ikifika jioni yanakuwa safi na nitarudi tena kutizama," alisema Kitwana.

Alisema mbali na majaa kuzagaa taka pia barabara mbalimbali za Wilaya ya Mjini sio safi, hivyo aliutaka uongozi huo kuwa na mpango mzuri wa usafishaji na uzoaji wa taka katika majaaa na barabarani.

Katika hatua nyingine, Kitwana aliitaka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), kuangalia vizuri uhalali wa mkataba wa kampuni ya usafi ya Green Weste Pro Ltd ili kuona uhalali wake wa kuipata kazi hiyo.

Wakati huohuo, Mkuu wa Mkoa ameuagiza uongozi wa Manispaa ya Mjini kusimamia tatizo la karo ya maji machafu katika nyumba za maendeleo za michenzani ili kuepusha athari za maradhi ya mlipuko.

Naye Meneja wa Kampuni ya Green Weste Pro Limited ya Dar es Salam, Erick Mark, alisema kampuni hiyo imekuwa ikifanya jitihada za kufanya usafi, lakini wananchi hawatoi ushirikiano wa kutosha.

Alisema wananchi wanatakiwa kuwa na utamaduni wa kuzihifadhi taka katika mifuko na kuzipeleka katika majaa na magari ya kampuni hiyo itazichukua kwa wakati na tatizo la kuzagaa litaondoka.

# Azaki zatakiwa kasi vita ya rushwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi, amezitaka jumuiya zisizo za kiserikali kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya udhalilishaji, rushwa na uhujumu uchumi.

Aliyasema hayo alipokuwa akifungua mkutano wa wanajumuiya zisizo za Serikali kuhusu kutoa maoni ya kurekebisha sheria mpya ya asasi zisizo za kiserikali. Alisema kufanya hivyo itaisaidia serikali dhidi ya mapambano ya vitendo hivyo pamoja na kuonyesha juhudi na utendaji wa jumuiya hizo kwa jamii.

Aidha, aliwataka wanajumuiya hao kutumia mkutano huo kutoa maoni yao yatakayosaidia kujenga utendaji mzuri pamoja na kuwa na sheria nzuri ambazo zitasaidia katika kuendesha jumuiya zao.

Mrajisi wa jumuiya zisizo za kiserikali kutoka Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na idara maalum za SMZ, Ahmed Khalid Abdallah, alisema afisi ya mrajisi imeona upo umuhimu wa kuifanyia marekebisho sheria ya asasi zisizo za kiserikali kutokana na sheria iliyopo sasa kupitwa na wakati na haiendani na kasi ya sasa ya kiutendaji wa jumuiya hizo.

# SMZ yaupa neno mradi wa viungo

**Na Rahma Suleima,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk, Haji Salim Khamis, amesema katika kukuza maendeleo ya Zanzibar, sekta binafsi zina mchango mkubwa iwapo zitafanya majukumu yake inavyostahiki kwa maslahi ya umma.

Aliyasema hayo alipokua akifungua mafunzo ya siku tano kwa mabwana shamba na mabibi shamba yenye lengo la kuwajengea uwezo wa kuandaa na kuratibu vyema shamba darasa kupitia wilaya tano za Unguja katika mradi wa viungo uliofadhiliwa ja Umoja wa Ulaya (EU) visiwani Zanzibar.

Alisema wakati Serikali ikiendelea na jitihada zake za kukuza uchumi wa Zanzibar, ni wazi kuwa wanategemea sana sekta binafsi kukuza ajira na kuongeza kipato kwa wananchi wake.

Alisema sekta ya kilimo ni miongoni mwa sekta muhimu Zanzibar, hivyo kila mmoja katika washiriki hao wa mafunzo wana wajibu wa kuhakikisha wanasikiliza na kuelewa vyema mafunzo hayo ili kuwanufaisha wengine katika jamii zao.

Sambamba na hilo, aliwataka watekelezaji wa mradi huo kuhakikisha wanasimamia vyema wajibu wao wakifahamu kuwa mategemeo makubwa ya Serikali kwa wananchi wake ni kupitia mradi huo.

Meneja mkuu wa mradi huo, Amina Ussi Khamis, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuwa wabunifu mara watakapomaliza masomo yao ya siku tano.

"Nyinyi mtakaopata mafunzo haya ni matumaini yetu kuwa mtakwenda kuwa wabunifu na kuwa chachu ya mabadiliko katika maeneo yenu," alisema.

Aidha, alisema utaratibu wa kuwapatia mafunzo mabwana shamba unalenga kuwafunza utaratibu mzuri wa shamba darasa, ambayo yatatumiwa kuwafundisha wanufaika wa mradi huo.

Baadhi ya washiriki hao kutoka wilaya tano za Unguja, walisema mafunzo hayo yamekuja wakati mwafaka ukizingatia mahitaji ya wakulima wengi kwenye maeneo yao wanayofanyia kazi.

Mize Juma, kutoka Wilaya ya Kusini Unguja, alisema baadhi ya wakulima wanashindwa kufanya vizuri katika kilimo kutokana na kukosa elimu bora ambayo ingewawezesha kufanya shughuli zao kwa weledi mkubwa.

Alisema kupitia mafunzo hayo, anaamini kuwa yatawajengea uwezo masuala ya kutunza na kuandaa shamba darasa.

Mradi huo wa viungo unatekelezwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) ofisi ya Zanzibar, chini ya ufadhili wa EU na unatekelezwa kwa miaka minne.

## HABARI PICHANI

# SAFARI YA MWISHO YA MAALIM SEIF SHARIF HAMAD



Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, baada ya kuusalia katika msikiti wa Ma'amour, Upanga, jijini Dar es Salaam jana kabla kuusafirisha kwenda Zanzibar. **PICHA: MIRAJI MSALA**




Mwili wa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, ukishushwa kwenye helikopta ya Jeshi la Wananchi Tanzania ( JWTZ), baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar jana, ukitokea jijini Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi na viongozi wengine wakijumuika na wananchi wa Zanzibar katika sala ya kuombea mwili wa Maalim Seif Sharif Hamad, ilioongozwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, katika viwanja vya Mnazi Mmoja. **PICHA: IKULU**



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akijumuika pamoja na wananchi wa Zanzibar katika sala maalum ya kusalia mwili wa Maalim Seif Sharif Hamad katika Viwanja vya Mnazi Mmoja. **PICHA: OMR**



Umati wa wananchi wa Zanzibar, wakiwa katika viwanja vya Mnazi Mmoja wakisubiri kuusalia mwili wa Maalim Seif Sharif Hamad. **PICHA: IKULU**




Sehemu ya waombolezaji waliofika katika viwanja vya Mnazi Mmoja wakipiga picha za kumbukumbu kwa kutumia kamera za simu. **PICHA: IKULU**



# ANCELOTTI: HAKUNA WA KUWAZUIA MAN CITY

**LIVEEPOOL, England**

KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti ameipongeza Manchester City na kuwathibitisha kwamba, watakuwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu England baada ya timu yake kukubali kichapo cha mabao 3-1 pale katika dimba la Goodison Park.

Man City imeongeza gepu la pointi hadi 10 dhidi ya majirani zao Manchester United waliopo nafasi ya pili baada ya ushindi huo wa Jumatano usiku, kwa mabao ya Phil Foden, Riyad Mahrez na Bernardo Silva.

Nyota wa Everton, Richarlison alifunga bao moja ambalo halikutosha kuwafanya Toffees hao kuepuka kichapo hicho cha pili mfululizo, baada ya kutoka kufungwa na Fulham 2-0, Jumapili.

City wameshinda mechi zao 12 za ligi zilizopita, 17 katika mashindano yote, na Ancelotti anaona hakuna wa kukizuia kikosi hicho cha Pep Guardiola kutwaa taji la Ligi Kuu msimu huu.

"Nafikiri hivyo. Ni ngumu sana kusema vinginevyo," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari.

"Man City kwa wakati huu wapo vizuri sana. Wana kikosi imara na chenye ubora wa hali ya juu, wako imara sana.

"Tulijaribu kupambana, lakini ilikuwa ngumu kwetu kupenya dhidi ya timu yenye wachezaji wenye ubora wa hali ya juu."

## MESSI ANATAKA MATAJI SIO FEDHA - LAPORTA



**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi hafikirii sana fedha, akili yake ni kutwaa mataji wakati hatima yake ikiwa haijulikani pale Barcelona, kwa mujibu wa mgombea urais, Joan Laporta.

Messi amekuwa akihusishwa sana na mabingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain na miamba wa Ligi Kuu England, Manchester City, huku mkataba wake ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, alijaribu kuondoka Camp Nou mwanzoni mwa msimu huu 2020-21, kabla ya kuamua kubaki.

Bado kuna mashaka juu ya majaliwa ya Messi baada ya Barcelona kuchezea kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa PSG kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16, Jumanne, Laporta ana matumaini ya kumbakiza nyota huyo mwenye umri wa miaka 33.

"Anachotaka ni kushinda mataji, hilo ndilo muhimu kwake," alisema Laporta akiiambia Sky Sport Italia.

"Habari ya mapenzi kati ya Messi na Barcelona ni moja kati ya habari nzuri sana kwenye soka.

"Anataka kupendwa, anastahili na anatakiwa kupewa thamani yake ambayo inamfanya ajisikie vizuri, lakini yeye si mtu wa kupenda fedha."

# MBAPPE: SIJAAMUA HATIMA YANGU PSG

**PARIS, Ufaransa**

BAADA ya kuwachapa Barcelona kwenye mechi yao ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16, mshambuliaji wa PSG, Kylian Mbappe, amesisitiza kuwa itakuwa ni ujinga kwake kufanya maamuzi ya hatima yake kwa kuzingatia mechi moja tu.

Barcelona walimaliza siku vibaya baada ya vijana wa PSG kuwakimbiza mchakamchaka kwa kuwashushia kichapo cha mabao 4-1, Jumanne wiki hii.

Licha ya kuanza vema kwa Messi kuwapatia bao la kwanza Barcelona, PSG walipindua meza wakati Mbappe aking'ara zaidi.

Mbappe alifunga mabao matatu 'hat-trick' na kuwafanya PSG waibuke kidedea, wakati akiwa anahusishwa zaidi na uhamisho wa kwenda Real Madrid au Liverpool.

Licha ya kusisitiza kuwa bado anafurahia kuwapo PSG, nyota huyu bado hajafanya maamuzi ya kusaini mkataba mpya klabuni hapo.

Akizungumza na RNC Sport baada ya mechi dhidi ya Barcelona, alisema itakuwa ni upuuzi kwake kufanya maamuzi kwa ajili ya mechi moja.

"Itakuwa upuuzi kuamua hatima yangu kwa sababu ya mechi moja tu. Ukweli katika kuangalia hatima yangu ya muda mrefu, ni kama nilivyosema wakati wote, nina furahia kuwa hapa na mechi kama hii zinakufanya uwe na furaha zaidi," alisema Mbappe.

Katika mchezo huo, Mbappe pia alijiwekea rekodi yake kwa kuingia kwenye orodha ya wachezaji walioifunga Barcelona mabao matatu.

Mbappe amekuwa mchezaji wa tatu kuwahi kuifunga Barcelona 'hat-trick' katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya Faustino Asprilla wa Newcastle na Andriy Shevchenko wa Dynamo Kyiv, zote zilikuwa mwaka 1997.

# DE BRUYNE

## SASA AREJEA DIMBANI



**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amethibitisha kwamba, kiungo wake, Kelvin De Bruyne amerejea mazoezini baada ya kuwa nje akiuguza majeraha kwa wiki kadhaa.

De Bruyne ameanza mazoezi na anatarajia kurudi kwenye kikosi cha Man City baada ya kushiriki mazoezi ya kikosi cha kwanza wiki hii.

Kiungo huyo wa kati amekuwa nje kwa karibu mwezi mmoja baada ya kuumia nyama za paja wakati wa ushindi wa 2-0 dhidi ya Aston Villa.

De Bruyne amekuwa akifanya mazoezi na kikosi cha kwanza cha Guardiola, na ana matumaini kwamba anaweza kujumuishwa kwenye kikosi cha mwishoni mwa wiki.

"Kevin ameshaimarika na amekuwa bora, kwa kweli amepata nafuu," alisema Guardiola.

"Alifanya mazoezi yote na wenzake na ninaamini ataweza kurudi uwanjani wiki hii."

# Neymar asikitika kuikosa Barcelona

**PARIS, Ufaransa**

NYOTA wa PSG, Neymar amesema alikuwa na hamu sana ya kurejea Camp Nou kupambana na timu yake ya zamani, Barcelona.

Neymar anatarajiwa kuwa nje ya uwanja kwa takriban mwezi mmoja baada ya kupata jeraha kwenye mechi ya Kombe la Ufaransa, na hiyo ilimfanya aikose mechi dhidi ya Barcelona.

Nyota huyo ni kama amekuwa na bahati mbaya na michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati PSG wakiwa wamecheza jumla ya mechi 10 kwenye hatua ya mtoano, yeye amecheza sita tu.

Katika ukurasa wake wa twitter akizungumzia mechi dhidi ya Barcelona, Neymar aliandika, "Mechi tatu nilizotamani zaidi kuzicheza."

Baada ya sekunde kadhaa aliifuta 'tweet' yake na kuitaja kama ilikuwa ni utani. Inakumbukwa nyota huyu alihusishwa sana na uhamisho wa kurejea Barca kabla ya suala hilo kubuma.

Barcelona walianza kwa kuongoza mechi dhidi ya PSG, kabla ya kibao kuwageukia na kujikuta wakimaliza mchezo kwa kichapo cha mabao 4-1.



# Pirlo aitaka Juventus kubadilika kuitoa Porto

**LISBON, Ureno**

KOCHA wa Juventus, Andea Pirlo, anakubali Juventus "wanahitaji kuonyesha kitu tofauti sana" kwenye mechi ya pili dhidi ya FC Porto ikiwa watataka kupenya kwenye hatua ya inayofuata ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Juventus waliruhusu bao katika dakika ya ufunguzi wa kila kipindi, lakini bao la Fredirico Chiesa la dakika za mwisho liliwapa tumaini kidogo kwa bao la ugenini.

"Mbinu tuliyotumia kwenye mchezo huu imetushuhudia tukilazimika kuukabili na kuupanda mlima kwa haraka sana. Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati ambao haujakamilika kuzingatia mchezo, wanakuadhibu," alisema



Pirlo akiiambia Sky Sport Italia.

"Tulifunga bao la ugenini, ambalo linatupa nguvu kwa mechi ya pili, ambapo kwa hakika utakuwa mchezo tofauti kabisa.

"Tulihisi tu wasiwasi kutoka mwanzo na tukafanya maisha kuwa magumu kwetu tangu mwanzo wa mchezo.

"Kwa kweli itakuwa Juve tofauti katika mechi ya pili, kwa sababu ikiwa tunataka kufuzu kwa raundi inayofuata, tunahitaji kuonyesha kitu tofauti sana."

Mechi ya pili itakuwa Turin Machi 9, mwaka huu na ushindi wa 1-0 utatosha kwa Juve kufuzu hatua inayofuata.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# HAALAND ATAJA HAT-TRICK YA MBAPPE KUMBEBA

●●●Ni wakati akiifungia Borussia Dortmund mabao mawili dhidi ya Sevilla Ligi ya Mabingwa huku...

**SIVILLE, Hispania**

ERLING Haaland amemshukuru nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe kwa kufunga 'hat-trick' iliyomhamasisha yeye kuifungia Borussia Dortmund mabao mawili dhidi ya Sevilla kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, uliopigwa Jumatano.

Haaland sasa amefikisha mabao 18 aliyofunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hadi sasa katika mechi 13.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 amefunga jumla ya mabao 41 katika mechi 42 tangu alipojiunga na miamba hao wa Ujerumani akitokea klabu ya Salzburg ya nchini Austria mwaka 2019, na amekuwa akihusishwa kutakiwa na klabu kama Real Madrid na Manchester City.

Baada ya kumwangalia Mbappe aking'ara mbele ya Barcelona wakati PSG wakiibuka na ushindi wa mabao 4-1 pale Camp Nou Jumanne, Haaland alisema alitumia kiwango cha nyota huyo kama hamasa kwake.

"Lilikuwa jambo zuri kufunga. Naipenda Ligi ya Mabingwa Ulaya na wakati nilipomuona (Kylian) Mbappe akifunga 'hat-trick' nilipata hamasa kubwa na namshukuru sana," alisema Haaland.

Kwa kufunga bao lake hilo la 10 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye mechi saba alizoichezea Dortmund, Haaland amefikia rekodi ya kufunga mabao kumi kwa haraka zaidi na kuipiku rekodi ya Roy Makaay ambaye alifunga mabao 10 katika mechi 10 wakati akiichezea Bayern Munich msimu wa 2003-04.

Haaland pia amekuwa mchezaji wa tano kufunga mabao mawili katika mechi tatu mfululizo za Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiungana na Filippo Inzaghi, Giovane Elber, Robert Lewandowski na Cristiano Ronaldo.

## KWA UFUPI

**COMAN ANUKIA MAN UNITED**

BAYERN Munich inahofia winga wa Ufaransa, Kingsley Coman mwenye umri wa miaka 24, huenda akashawishika kujiunga na Manchester United kwa sababu ya mshahara walioahidi kumpa. ***(Bild, via Mail)***

**CEBALLOS KUFUNGWA ARSENAL**

ARSENAL inataka kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Dani Ceballos mwenye umri wa miaka 24, na mlinda mlango wa Australia, Mat Ryan mwenye miaka 28, kwa makubaliano ya kudumu msimu huu. Wawili hao sasa hivi wanacheza kwa 'Washikabunduki' hao kwa mkopo kutoka Real Madrid na Brighton. ***(Sun)***

**CAVANI HATAKI KUONDOKA**

STRAIKA wa Manchester United na Uruguay, Edinson Cavani, anataka kubakia pale Old Trafford kwa msimu mwingine zaidi. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alijiunga na 'Mashetani Wekundu' hao baada ya kufikiwa kwa makubaliano ya mwaka mmoja msimu uliopita. ***(Telegraph)***

**BEI YA MBAPPE YATAJWA**

KLABU ya Paris St-Germain imeweka euro milioni 200 kama ada wanayoitaka kwa mshambuliaji wao, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, ambaye anafuatiliwa na Real Madrid, Liverpool, Manchester City na Juventus. ***(La Parisien)***

**ARSENAL KUMUUZA LACAZETTE**

STRAIKA wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29, ni mmoja kati ya wachezaji wa Arsenal ambaye huenda akauzwa mwishoni mwa msimu huu kama sehemu ya kupunguza gharama. ***(Sun)***

**MBAPPE KATOSWA BARCELONA**

BARCELONA ilitaka kumsajili Kylian Mbappe mwaka 2017, lakini badala yake ikaamua kumnunua mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 22 kutoka Borussia Dortmund. ***(Mirror)***

**LAPORTA KUMBAKIZA MESSI**

MGOMBEA urais wa Barcelona, Joan Laporta, ameahidi kufanya "kila linalowezekana" kumshawishi mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, kubakia klabuni hapo. ***(Sky Sports)***

**MADRID INAMTAKA TORRES**

REAL Madrid inafikiria kumsajili mlinzi wa kati wa Villarreal raia wa Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 24. ***(Goal)***

**HENRY, VIEIRA HAO BOURNEMOUTH**

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Thierry Henry na Patrick Vieira wanatajwa kwamba, wapo kwenye nafasi nzuri ya kupewa mikoba ya ukocha kule Bournemouth. ***(Talksport)***

**WATATU KUONDOKA ARSENAL**

MLINZI wa Brazil, David Luiz mwenye umri wa miaka 33, kiungo wa kati wa Uruguay, Lucas Torreira mwenye, 25, na kiungo wa kati wa Ufaransa, Matteo Guendouzi, 21, pia wanaonekana kuwa tayari kuondoka Arsenal. ***(Star)***

**SUAREZ ATAZAMA KUSTAAFU**

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid na Uruguay, Luis Suarez mwenye umri wa miaka 34, amesema ataamua muda mwafaka wa kustaafu, lakini haitakuwa hivi karibuni. ***(ESPN)***

HABARI MICHEZO

# MTIBWA YALIA UWANJA WA JAMHURI KAMA WA UGENINI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Mtibwa Sugar, Thierry Hitimana, amesema Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro ambao wamekuwa wakiutumia kama wa nyumbani, umegeuka kuwa ni kama uwanja wa ugenini kwao.

Akizungumza kutoka mjini Morogoro baada ya mechi kati ya timu yake ya Mtibwa Sugar dhidi ya Ihefu kumalizika kwa sare ya bao 1-1 uwanjani hapo juzi, Hitimana alisema walicheza kwenye uwanja huo bila hata kuufanyia mazoezi, tofauti hata na wageni wao ambao walifanya mazoezi kwenye uwanja huo.

"Uwanja huu sisi ni kama tuko ugenini tu, huwa tunakuja wakati wa mechi, na hata kwenye mechi hii hatujafanya mazoezi hapa, lakini wenzetu Ihefu jana walifanya hapa, hiyo imekuwa shida kidogo," alisema kocha huyo wa zamani wa timu za Biashara United na Namungo FC.

Hata hivyo, alisema kuna baadhi ya makosa ambayo ameyaona kwenye mechi hiyo na ameahidi kuyarekebisha kwenye mechi zinazofuata.

Mtibwa imekuwa ikitumia Uwanja wa Manungu Complex kwa misimu kadhaa, lakini msimu huu inautumia kwa kufanyia mazoezi tu, huku ikitumia Uwanja wa Jamhuri Morogoro kwenye mechi zake za nyumbani.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, alisema alikwenda Morogoro huku akijua anakwenda kupambana na timu ya aina gani, inacheza vipi na hata wachezaji anaokwenda kucheza nao, hivyo haikumpa wakati mgumu sana, ingawa mechi haikuwa rahisi. "Nilijua nakwenda kucheza na timu ya aina gani, ina wachezaji gani na mfumo gani. Ni kweli kwa asilimia kubwa walicheza kama nilivyotarajia, ingawa kocha Hitimana kuna vitu ambavyo aliviongeza na ikabidi na mimi kipindi cha pili nibadilike," alisema Katwila.

Ikumbukwe kuwa Katwila alikuwa kocha wa Mtibwa Sugar, kabla ya kuachana na timu hiyo na kujiunga na Ihefu.

Kwa matokeo hayo, Ihefu imefikisha pointi 17 kwa mechi 20 ilizocheza, ikikamata nafasi ya 16, huku Mtibwa ikiwa nafasi ya 11 ikiwa na pointi 23 nafasi hizo zikiwa ni kabla ya mechi za ligi hiyo zilizopigwa jana.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas (kushoto) na Mwenyekiti wa Klabu ya Namungo, Hassan Zidadu, wakionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 120, baada ya kampuni hiyo kuingia mkataba wa kudhamini tena kwa kipindi cha mwaka mmoja. Katikati anayeshuhudia ni mshambuliaji wa timu hiyo, Stephen Sey. **MPIGAPICHA WETU**

# SportPesa yaidhamini tena Namungo kwa mil. 120/-

**Na Mwandishi Wetu**

MAFANIKIO ya Klabu ya Namungo kwenye soka la Tanzania na sasa Kombe la Shirikisho Afrika, yameivutia Kampuni ya Michezo na Burudani ya SportPesa, hivyo kuamua kuongeza mkataba wa mwaka mmoja wa kuidhamini klabu hiyo kutoka Ruangwa mkoani Lindi, imeelezwa.

Namungo ambayo msimu uliomalizika ilicheza fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba iliyolitwaa taji hilo, imetinga hatua ya mchujo kuwania kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu ambapo itacheza mechi mbili dhidi ya CD de Agosto ya Angola hapa nchini kuwania nafasi hiyo.

Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas, akizungumza wakati wa kusaini mkataba wa udhamini na klabu hiyo jijini Dar es Salaam juzi, alianza kwa kuipongeza Namungo kwa kujiendesha vizuri na kuhakikisha timu inafanya vizuri barani Afrika na kuipa sifa nzuri si Tanzania pekee bali pia hata SportPesa.

"Hii ndio sababu iliyotufanya kuendelea kuwadhamini Namungo, ukiangalia vizuri klabu ya Namungo tangu ianze mpaka sasa unaweza kuona ni jinsi gani ilivyo na moyo wa kujituma na kuhakikisha inafika mbali.

"Tunawatakia kila la kheri katika mechi zinazoendelea, kumbuka kuwa kwenye mkataba huu kuna zawadi ambazo tutawapa endapo timu itafanya vizuri katika hatua za roba fainali, nusu fainali na ubingwa," Tarimba alisema.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Klabu ya Namungo, Hassan Zidadu, alisema: "Kwanza kabisa ningependa kuwashukuru sana SportPesa kwa kutupokea kwa mikono miwili na kuendeleza mkataba wetu kwa mwaka mwingine tena. Hii ni ishara ya kutukubali sisi kama klabu na kujiunga katika maendeleo yetu ili kuboresha uendeshaji wa klabu hii.

"Kama klabu tunaahidi kuendeleza ushirikiano huu kwa kufanya vizuri maana nyinyi ni kama wawekezaji mkiwa na nia kubwa ya kuhakikisha klabu inajiendesha na kufikia malengo yake.

"Kwenye Kombe la Shirikisho Afrika timu imeingia kwenye hatua ya timu 32 bora barani. Mafanikio kama haya ndio yanayotufanya tuendelee kufanya vizuri na nathubutu kusema bila SportPesa tusingefika hapa. Tunajivunia sana kwa kweli."

Huu utakuwa ni mjumuisho wa miaka miwili tangu kumalizika kwa mkataba wa kwanza kati ya SportPesa na Namungo.

SportPesa pia ni wadhamini wakuu wa Klabu za Yanga na Simba na kwa sasa wameongeza mkataba wa mwaka mmoja kwa klabu ya Namungo ambayo nayo inashirika katika Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa katika nafasi ya 13 na pointi 21 zilizotokana na mechi 16, kabla ya matokeo ya mechi za jana ambapo timu zingine zilikuwa zinacheza mechi ya 20.

# Rais ZFF ajiuzulu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

RAIS wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu, amejiuzulu nafasi yake hiyo, imeelezwa.

Katika barua yake aliyoiandika kwa shirikisho hilo, ameeleza kuwa kachukuwa maamuzi hayo kwa maslahi mapana ya soka la Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Pandu alisema ameamua kupumzika ili kufanya shughuli zake nyingine, lakini pia ataendelea kutoa mchango wake katika safari ya soka la Zanzibar.

Pandu amedumu katika nafasi hiyo takriban mwaka mmoja na nusu tangu alipochaguliwa Juni 2019 na katika historia ya soka la Zanzibar anakuwa rais wa tatu kujiuzulu nafasi hiyo.

# Ligi Zanzibar yasimama kupisha maombolezo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limesimamisha ligi zote kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya ili kupisha maombolezo kifo cha Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ZFF pamoja na Bodi ya Ligi jana kwa vyombo vya habari, imeeleza kuwa kuendelea kuchezwa kwa ligi hizo ni mpaka watakapofanya mawasiliano na wizara husika ya michezo visiwani hapa.

**Akizungumza na gazeti hili Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi, Sheha Mohamed, alisema shughuli itakayoendelea katika soka la Zanzibar kwa sasa ni klabu kuendelea kuboresha vikosi vyao kupitia usajili wa dirisha dogo baada ya dirisha kufunguliwa jana, Februari 18.**

Aidha, alisema awali Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa pili ilipangwa kuanza kesho, hivyo kwa sasa wanasubiri kupata taarifa mpya ya tarehe rasmi ya kurejea kwa ligi hiyo baada ya msiba huo mzito ulioikumba Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Hata hivyo, alizisisitiza klabu kufanya usajili kwa wakati ili kuepusha usumbufu kwa kuwa usajili huo kwa sasa unafanyika kwa njia ya mtandao.

# Michezo

Ijumaa Februari 19, 2021

Nipashe




HAALAND ATAJA HAT-TRICK YA MBAPPE KUMBEBA HABARI UK 22

## HAA! SI PENALTI?...



Cristiano Ronaldo akishangaa kitendo cha mwamuzi kutomzawadia penalti baada ya kuchezewa madhambi ndani ya 18, wakati wakiwa nyuma kwa mabao 2-0 dhidi ya FC Porto kwenye mechi ya 16-bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kabla ya Federico Chiesa kuipatia Juventus bao la kufutia machozi dakika ya 82 na kufanya matokeo kuwa 2-1, ambayo yanawapa matumaini ya kuweza kusonga mbele timu hizo zitakaporudiana Turin, Italia. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YABISHA HODI MLANGONI KWA YANGA

Ni baada ya Morrison kuwakera Biashara United kwa kuipa pointi tatu huku...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, wameendeleza rekodi safi ikicheza kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma mkoani Mara dhidi ya Biashara United, ilipopata ushindi wa bao 1-0 kwenye mfululizo wa ligi hiyo, hivyo kuwapigia hodi watani zao, Yanga waliopo kileleni.

Hii ni mara ya tatu kwa mabingwa hao kupata ushindi tangu timu hiyo ya Biashara United ipande na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2018/19, ambapo ilifungwa mabao 2-0 Aprili 27, 2019, yakifungwa na John Bocco, na Septemba 29, 2019, msimu wa 2019/20, yakifungwa na Meddie Kagere na Miraji Athumani.

Alikuwa ni Bernard Morrison aliyepeleka pointi zote tatu Msimbazi, alipofunga bao hilo pekee dakika ya 21, ambalo limeifanya Simba kufikisha pointi 42 katika nafasi ya pili baada ya mechi 18, hivyo kuikaribia Yanga mlangoni ambayo ipo kileleni ikiwa na alama 46 zilizotokana na michezo 20.

Kwa msimamo huo jinsi ulivyo, endapo Simba itashinda mechi zake za viporo, itafikisha pointi 48, hivyo kuwapiku watani zao kwa alama mbili zaidi.

Bao hilo lilitokana na kizaazaa kilichotokea kwenye lango la Biashara United, Thadeo Lwanga akipiga shuti lililookolewa na mguu na kipa James Ssetuba, lakini ukarudisha tena kwenye eneo la hatari na kumkuta Hamis Ndemla aliyemmegea pande Morrison akiwa yeye na kipa, akaujaza wavuni kwa shuti dhaifu la kiufundi.

Linakuwa ni bao la tatu la Morrison msimu huu, akijiunga na Simba kutokea Yanga, Februari 4, mwaka huu akifunga bao la ushindi kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma dhidi ya Dodoma Jiji, Simba ikishida 2-1, bao lake la kwanza akifunga Novemba 21, mwaka jana kwenye mechi ambayo Simba ilishinda mabao 7-0 dhidi ya Coastal Union katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Mchezaji aliyesajiwa kipindi cha dirisha dogo akitokea FC Platinum ya Zimbabwe, Perfect Chikwende alikosa bao la wazi, akiwa anatazama na kipa Ssetuba, lakini alipiga shuti lililopaa juu dakika ya 44 ya mchezo.

Kipindi cha pili timu ziliendelea kucheza mchezo kama wa kipindi cha kwanza, wa kutumia nguvu na mipira mirefu kutokana na hali ya uwanja iliyokuwa na nyasi ndefu, pasi fupi zikikwama kufikia walengwa.

Dakika ya 50, Aishi Manula aliruka mbizi kuuokoa mpira wa krosi iliyokuwa inakwenda kutua kwenye kichwa cha Deogratius Judika, lakini mpira huo ulimkuta Mghana Christina Zigah akapiga shuti lililotoka nje kidogo ya lango.

Morrison angeweza kuipatia Simba bao la pili dakika ya 57 kwenye nafasi ambayo ilikuwa ngumu kukosa kuliko kupata, alipoukuta mpira ukiwa hatua chache tu kwenye lango tupu la Biashara United, lakini alipiga kwa nguvu mpira ukapaa juu.

## KAZE ATOA SABABU KAGERA KUWASHIKA

**Na Saada Akida**

HUKU akimtetea kiungo mkabaji Zawadi Mauya kuwa si kwamba alishindwa kutekeleza kile alichokitaka, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema sababu ya kushindwa kupata matokeo dhidi ya Kagera Sugar juzi, ni kutokana na wachezaji wote kutojiamini katika mchezo huo wa Ligi Kuu Bara.

Lakini wakati Kaze akisema hayo, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kupata pointi moja na mabao 3 mbele ya Yanga ambayo inaongoza msimamo wa ligi hiyo.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, timu hizo zilitoka sare ya mabao 3-3, huku Yanga ikitokea nyuma na kusawazisha kila ilipofungwa.

Kaze alisema hawezi kumtupia lawama mchezaji mmoja kwa sababu wote hawakufanya kile alichowaelekeza dakika 45 za kipindi cha kwanza kwa kufika kwenye eneo lao huku mabeki wa pembeni nao wakiwaruhusu wapinzani wao kupiga mipira ya krosi.

“Mpira una matokeo matatu, kushinda, kushindwa na sare, ukiangalia katika mechi ya leo (juzi), wachezaji wangu hawakufanya kile ambacho niliwapa mazoezini hii ni baada ya kukosa umakini kwenye nafasi tulizotengeneza uwanjani.

“Tumeruhusu Kagera kufika kirahisi katika eneo letu, huku mabeki wa pembeni nao hawakufanya kazi yao kwa kuruhusu wapinzani wetu kutumia madhaifu yetu kupata pointi moja na mabao matatu,”alisema Kaze.

Alisema kutomwanzisha Mukoko Tonombe katika mchezo huo ni kwa sababu alihitaji kufanya mzunguko wa wachezaji wake wote kulingana na ratiba ya mechi zao kubana na kumpa muda wa kupumzika.

“Katika wiki tuna mechi tatu, lazima kuwapo kwa mzunguko hakuna mchezaji ambaye atacheza dakika 90 zote na kutakiwa kupumzika, laiti kungekuwa na ruhusa ya kufanya mabadiliko wachezaji saba, nina imani katika kipindi cha kwanza ningewapumzisha wachezaji wawili hadi watatu,” alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042